Tanzania kupatiwa tril. 1.4/- malaria, TB

UKURASA 3



**NEEMA** zaidi ajira 137,294 sekta ya afya

UKURASA 4



**RAIS** Ruto anusurika kifo ajalini

UKURASA 19


# Nipashe

Alhamisi Februari 1, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581573

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




**PEP KUAMUA KUHUSU MUSTAKABALI WAKE**

UKURASA 22

# Simulizi za wabunge madhila unyanyasaji

**WAELEZA** machungu waliyopata walipogombea, wapongeza kuwa kosa kisheria ... *Endelea ukurasa wa 2*



**" Nimeanza kugombea jimbo tangu mwaka 2005. Nakutana na haya mambo ambayo wengi wanayachukulia ni madogo, la hasha! Manyanyaso ni makubwa sana wakati tunapogombea." - Anne Malecela**



**"Vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake wanapogombea ni vikubwa. Nilitukanwa kwa kuambiwa nina nyonyo moja na mmoja wa kiongozi." - Sophia Mwakagenda.**




**"Mwanamke ukitukanwa unafundishwa vita. Tusilale mimi nimeshaonyesha njia, unalia nini? Tumepata fursa sawa twende tukagombee." - Jesca Msambatavangu.**



**"Kuna wanawake wameshindwa kuchaguliwa kwa sababu fulani na kwamba hiyo inatokana na kuwapo mfumo dume." Miraji Mtaturu**



**"Kumekuwa na matusi sana kwa wagombea wawapo kwenye uchaguzi... adhabu inayopendekezwa ni ndogo." Zelemani Zedi**



**"Hata wanaume wakipanda majukwaani wako wanaowaita mashoga."- Hadija Taya (Keisha)**

UKURASA WA 4

## SPIKA ATAKA FEDHA KUTENGENEZA BARABARA ZILIZOATHIRIKA NA MVUA

SPIKA wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, ameiagiza serikali fedha zinazopelekwa kufungua barabara zilizoathiriwa na mvua, kipaumbele kitolewe kwanza...

UKURASA WA 7

## MADUKA YA BIASHARA MWENGE YAANZA KAZI

BAADA ya ukimya wa muda mrefu, hatimaye maduka ya biashara katika kituo cha mabasi cha Mwenge, Kinondoni mkoani Dar es Salaam...

# Shehena sukari yanaswa ikiingizwa kwa magendo

UKURASA 2

## Tofauti majina yaibua mvutano maziko ya mtoto

UKURASA 3

**MICHEZO** BENCHIKHA AWEKA MSIMAMO WAKE KWA INONGA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Miradi, Mhandisi Ramadhani Mtindasi (kulia), kuhusu mradi wa usafi wa mazingira uliohusisha ujenzi wa vyoo vya kisasa vya kijamii katika maeneo ya masoko, wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya Chuo cha Maji yaliyofanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Simulizi wabunge madhila unyanyasaji

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wamesimulia madhila ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia waliyokutana nayo wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Kutokana na kutawala kwa madhila hayo, wabunge hao wamepongeza muswada wa Sheria ya Uchaguzi kuweka bayana kwamba unyanyasaji huo ni kosa kisheria.

Wakichangia mjadala wa Muswada wa Sheria ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023, wabunge hao walisema hatua ya kuwekwa kipengele cha kosa la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia, litakomesha matukio hayo wakati wa uchaguzi.

Akichangia muswada huo jana bungeni jijini hapa, Mbunge wa Same Mashariki, Anne Kilango Malecela (CCM), alisema anaamini sheria inayotungwa hivi sasa itakuwa mwarobaini wa tatizo hilo.

Malecela alisema tangu muswada huo ulipowasilishwa bungeni, kilichomgusa ni vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia kuanza kutambulika kuwa kosa la uchaguzi.

"Mimi ni mwathirika, ni mbunge wa jimbo mwanamke. Nimeanza kugombea jimbo tangu mwaka 2005. Nakutana na haya mambo ambayo wengi wanayachukulia ni madogo, la hasha! Manyanyaso ni makubwa sana wakati tunapogombea.

"Niipongeze kamati kwa kuliona jambo hili na kuliweka kwenye sheria inayotungwa. Natambua kikamilifu ziko sheria zinazosimamia ukatili wa kijinsia lakini hii ni mahususi kwa wanyanyasaji katika uchaguzi," alisema na kuongeza:

"Hatuwezi kutumia ile inayoendelea ya wote, mtanisamehe nizungumze kwa mifano. Mniwie radhi, kina baba mniwie radhi, nitoe mfano ili serikali ielewe kwa nini mama Anne Kilango anang'ang'ania kwamba udhalilishaji na ukatili kwenye uchaguzi uchukuliwe kama mnavyochukulia rushwa."

Alisema mwaka 2005, wiki ya pili wakati anagombea Same Mashariki, akiwa katika kampeni za uchaguzi mkuu, mgombea mwenzake alisimama jukwaani na kumzungumzia (Malecela) masuala ya ndoa yake hali ambayo ilimfedhehesha.

"Wakati narudi nyumbani siku hiyo jioni, nikakuta wanawake wa CCM wamekimbilia nyumbani, nikawafuata wakasema mwenzio amesema hufai ubunge kwa sababu unampeleka mume wako polisi," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema alilazimika kumpigia simu Mwenyekiti wa Uchaguzi na Mkurugenzi wa Uchaguzi ili ambadilishie ratiba ya eneo la kufanyia kampeni ili aende katika eneo ambalo mpinzani wake alimdhalilisha ili kuwaeleza wananchi ukweli sababu ya yeye kumshtaki mume wake polisi.

"Mwenzangu (mume wake) alinikuta napiga pasi nguo za kwenda kanisani, akaichukua akanichoma mgongoni, ikaondoka na nyama. Kwa kitendo hicho, lazima niende nikaripoti polisi nikapewa Pf3 (fomu namba tatu ya polisi) nikaenda hospitalini. Sasa nirudi nieleze wananchi kwenye mkutano sababu ya kumpeleka polisi, nikafungua vifungo nikawaonyesha mgongo, wakaona kidonda kile," alisema.

Alisema alilazimika kutoa mfano huo ili serikali ione umuhimu wa unyanyasaji wa ukatili wa kijinsia unavyojitokeza katika kampeni, jambo ambalo ni sawa na rushwa.

"Wanawake tunateseka, msidhani hawa wanawake hapa ndani hawataki kugombea majimbo. Wanataka lakini wana hofu ya kuogopa haya manyanyaso, wote wana uwezo hivyo suala la unyanyasaji msilichukue kwa udogo serikali.

"CCM tuna mgombea mwanamke katika uchaguzi. Wanawake tuna wivu uliopitiliza na mgombea wetu, hatutakubali tukakutane na lugha hizi, wakati mgombea wetu anastahili na amefanya kazi nyingi," alisema.

Anne alisema: "Nimesema ili serikali muone namna tunavyoteseka, nchi itafikiaje usawa wa kijinsia kama majukwaa yanatumika kufanyia ukatili wagombea? Wanawake wana hofu na wanayokutana nayo iwapo sheria itaweka katazo kubwa wote watagombea majimbo," alisisitiza. Baadaye, hoja hiyo ilitolewa taarifa na Mbunge wa Sikonge, Joseph Kakunda (CCM), ambaye alimweleza mchangiaji kuwa katika kura za maoni mwaka 2020, aliyegombea ubunge naye alipitia madhira ya unyanyasaji.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, alisema vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake wanapogombea ni mkubwa, huku akifichua siri ya yeye kutukanwa kwa kuambiwa ana nyonyo moja na mmoja wa viongozi.

"Mimi sikujali kwa sababu ninasaidiwa na familia yangu. Leo hii siji bungeni kunyonyesha, tumekuja kufanya kazi ya wananchi. Sasa maneno machafu kwenye uchaguzi yawekewe msisitizo mkali wa kuwakataza wanawake kunyanyaswa," alisema.

Mwakagenda alipongeza jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, alizofanya za kuleta muswada huo ili ujadiliwe na hiyo inaonyesha kuwa wanawake wanaweza.

Mbunge wa Iringa Mjini (CCM), Jesca Msambatavangu, alisema wakati anagombea kuna mtu alimtukana akimwambia anawezaje kuchaguliwa kuwa mbunge wakati hana mume.

"Nikajibu tu jukwaani, huyo unayelalamika kwamba sina mume, yeye ndiye mwanamume, katoe posa Kamati Kuu ya CCM, njoo unioe; vinginevyo utakuwa na matatizo ya kiume.

"Mwanamke ukitukanwa unafundishwa vita, tusilale mimi nimeshaonyesha njia, unalia nini? Simama maana tumepata fursa sawa twende tukagombee, tuitetee nchi," alisema Msambatavangu.

Akiunga mkono pendekezo la kuwamo kosa hilo, Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, alisema kuna wanawake wameshindwa kuchaguliwa kwa sababu fulani na kwamba hiyo inatokana na kuwepo mfumo dume ambao sheria hiyo inapaswa kuondoa.

Kadhalika, Mbunge wa Bukene (CCM), Seleman Zedi, alisema unyanyasaji wa kijinsia katika kampeni za uchaguzi, kwa wajumbe ni kweli zipo na imekuwa kero mara zote.

"Kumekuwa na matusi sana kwa wagombea wawapo kwenye uchaguzi, hivyo muswada huu utasaidia na kutambua kama suala hilo ni kosa linalotakiwa kuwa na adhabu ambayo imependekezwa ni faini ya Sh. milioni mbili au milioni tano.

"Nashauri wafungwe miaka miwili au mitano maana faini mtu anaweza kulipa ili atolewe, hivyo kosa likaendelea kutendeka," alisema Zedi.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Hadija Taya (Keysha), alisisitiza umuhimu wa jinsia zote kupewa fursa sawa na kutolea mfano kuwa hata wanaume wakipanda majukwaani wapo wanaowaita mashoga.


**NAFASI YA KAZI**

KAMPUNI YA MADAWA ILIYOPO DAR ES SALAAM INATAFUTA MTU WA MAUZO AWE MWANAMKE AU MWANAUME.

PIGA SIMU NAMBA: +255 713 786 300


# Sukari kilo 1,650 yanaswa ikisafirishwa kwa magendo

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kikosi cha Wanamaji jijini Dar es Salaam, limekamata kilo 1,650 za sukari zilizokuwa zikisafirishwa kimagendo kupitia Bahari ya Hindi zikitokea bandari bubu Zanzibar.

Taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa kikosi hicho, ACP Moshi Sokoro, ilisema sukari hiyo ilikamatwa Januari 11, mwaka huu, katika operesheni iliyoendeshwa kwa kushirikiana na maofisa forodha maeneo ya Kunduchi, wilayani Kinondoni.

Alisema katika operesheni hiyo walikamata majahazi mawili ambayo hayakuwa na namba za usajili, yakiwa yamebeba sukari viroba 550 vya kilo 50 kila kimoja.

"Jahazi moja la MV Kalunde, liliongozwa na nahodha Aman Mwalimu, akiwa na wenzake watatu lilibeba viroba 300 na SV likiongozwa na Zamiri Hamisi na wenzake watatu lilibeba viroba 250. Na vielelezo vimekabidhiwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa taratibu za kiforodha," alisema ACP Sokoro.

Katika hatua nyingine, alibainisha kuwa wamefanikiwa kuwakamata watuhumiwa watano wakiwa na mbolea aina ya Ammonium salfet kilo 200 na vilipuzi 443 vya aina mbalimbali na kwamba hatua za kuwafikisha watuhumiwa hao mahakamani zinaendelea.

Aidha, alisema Januari 9, mwaka huu, maeneo ya Feri Kigamboni, walimkamata mtuhumiwa Daniel Richard (35) kwa tuhuma za kujifanya mtumishi wa umma, kwa muda mrefu akiwatapeli wavuvi na kujipatia fedha kwa kujifanya askari polisi Kikosi cha Wanamaji.

ACP Sokoro alibainisha kuwa mtuhumiwa huyo alikuwa akiwalaghai wavuvi kwamba watakapokamatwa kwa kosa lolote atawasaidia na kwamba ameshtakiwa pia kwa kosa la kijipatia Sh. 150,000 kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa mvuvi ambaye ana kesi inayoendelea kituo cha polisi Wanamaji, jijini Dar es Salaam.

"Jeshi la Polisi Kikosi cha Wanamaji tunaamini mafanikio haya ambayo yanapatikana kutokana na operesheni mbalimbali ni kutokana na ushirikiano mzuri baina ya wananchi na jeshi, hivyo tunatoa wito ushirikiano huu uendelee ili kuhakisha kwamba bahari na maziwa yanakuwa sehemu salama, tutaendelea kushirikiana na vyombo vyote vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha uhalifu unatokomezwa," alisema ACP Sokoro.

Pia, alitoa onyo kwa wote wanaojihusisha na uhalifu katika bahari na maziwa ikiwamo wa uvuvi haramu na kukwepa ushuru wa forodha, kuachana na tabia hiyo na kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi, akisisitiza kwamba kinyume na hapo sheria itachukua mkondo wake kwa wote watakaobainika.

## HABARI KITAIFA



Mratibu wa Mtandao wa Accelerate Africa Tanzania, Pendo Lema (kulia), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa mashindano maalumu kwa ajili ya wajasiriamali watakaochuana ili kupata nafasi ya kuhudhuria mkutano mkubwa wa wajasiriamali na uwekezaji utakaofanyika Abu Dhabi mwezi Mei kwa uratibu wa mtandao huo na Shirika la AIM Startups. Kushoto ni Mratibu Msaidizi, Junior **Mushi. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali kufadhiliwa 'AIM Congeress 2024' Dubai

**Na Christina Mwakangale**

WAJASIRIAMALI 20 wanaochipukia na wabunifu kwenye sekta tofauti nchini ikiwamo afya, wanatarajia kushindanishwa ili kumpata mshindi atakayefadhiliwa kuhudhuria mkutano 'AIM Congress 2024' unaotarajiwa kufanyika Abu Dhabi (Falme za Kiarabu) Mei, mwaka huu.

Mratibu wa mtandao huo nchini, Pendo Lema, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa usaili unaendelea kwa wajasiriamali na kujiandikisha kabla ya Februari 16, 2024.

Alisema shindano hilo litawapa washiriki nafasi nzuri ya kuonesha ubunifu wao na teknolojia mbalimbali zenye kuleta mageuzi katika sekta hiyo nchini.

"Kama ndio umeanza tu au ndio umeanza kushika kasi kidogo katika biashara yako, hii ndio hatua itakayokusaidia kukuza biashara yako zaidi," alisema Pendo.

Akizungumzia baadhi ya faida za shindano hilo, alisema washiriki watakutanishwa na wataalamu mbalimbali na pia wadau wenye maamuzi ya kusaidia wajasiriamali wanaoanza kupiga hatua.

Kadhalika, alisema washiriki watapata nafasi ya kubadilishana uzoefu na wajasiriamali mbalimbali, wabia na waelekezaji ambao watawapa ushauri na mawazo mbalimbali ya namna ya kupiga hatua, kupata fursa na kutafuta mitaji.

"Mshindi wa shindano hili, atapata faida nyingi ikiwamo kuaminika na kuvutia uwekezaji. Vigezo vya kushiriki alisema ni lazima biashara iwe ni changa au iliyoanza muda sio mrefu, iwe na wafanyakazi angalau watano, iwe katika sekta ya teknolojia, iwe na muundo wa kibiashara wa kibunifu na pia iwe na angalau mtaalamu mmoja katika masuala ya teknolojia."

Accelerate Africa inaundwa na nchi zaidi ya 20 Afrika.

# Tofauti majina yaibua mvutano maziko mtoto

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TAHARUKI imeibuka katika maziko ya mtoto Amani Mfoi (3), anayedaiwa kuuawa kwa kuchinjwa na baba yake mzazi, Amedeus Mfoi (25) kwa kumtenganisha kichwa na kiwiliwili baada ya majina kutofautiana kwenye msalaba.

Taharuki hiyo ilisababisha ndugu wa upande wa mama wa marehemu, Gloria Pallangyo, kutishia kuondoka katika maziko hayo yaliyofanyika Murombo nyumbani kwa babu mzaa baba Isack Mfoi.

Akizungumza wakati wa tafrani hiyo, babu mdogo wa marehemu upande wa mama, Simon Mkwaju, alisema anaishi mkoani Manyara na marehemu ni mtoto wa kaka yake anamfahamu kwa jina la Amani.

"Tunachoshangaa hapa tunaona mambo ya ajabu, mtoto tunamfahamu kwa jina la Amani ambalo ndilo jina limeandikwa polisi na cheti cha kuzaliwa, lakini tunaona msalaba umekuja umeandikwa John, huku picha iliyotangulia na msalaba imeandikwa Amani sasa mambo gani.

"Tunaambiwa jina la John la ubatizo, lakini tukizika kwa msalaba ulioandikwa John tunatofautiana na taarifa za polisi, maana jina la marehemu limeandikwa Amani, hawa kisheria ni watu wawili tofauti, kama hawarekebishi tunaondoka hatushiriki mazishi haya," alisema.

Babu wa marehemu upande wa baba anayetuhumiwa kumuua mtoto huyo, Mfoi ambaye ni balozi wa nyumba kumi, alisema majina yote ni ya mjukuu wake na alimpa mwenyewe na Kichaga ni jambo la kawaida mtu kuwa na majina matatu la nyumbani, ubatizo na la ukoo.

"Mimi ndio nilimpa jina la Amani na John sasa kama kumtafuta aliyempa majina haya mtoto huyu wanitafute mimi na kawaida kwetu Wachaga kutoa majina matatu, na nawashangaa wanachong'ania ni nini wakati mimi ndio nilimpa majina haya," alisema.

Hata hivyo, baada ya taharuki hiyo upande wa baba wa marehemu ulitumia hekima kufuta jina la John kwenye msalaba huo na kuandika Amani.

Baaada ya maziko hayo, upande wa mama wa marehemu haukushiriki chakula cha safari ya mwisho ya mtoto wao, huku babu mzaa baba wa marehemu akisema chakula kimeliwa na watu na kimeisha.

Mtoto huyo aliuawa Januari 23, mwaka huu, majira ya saa 12:00 jioni huko Mtaa wa Murieti, Tarafa ya Elerai katika Jiji la Arusha kwa kutenganishwa kichwa na kiwiliwili, huku kichwa kikihifadhiwa katika ndoo na kiwiliwili kwenye nyingine kubwa na kufunikwa.

Akitoa taarifa hiyo baada ya tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi ACP, Justine Masejo, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na anashikiliwa na jeshi hilo akisubiri hatua zaidi za kisheria.

# Tanzania kupata trilioni 1.4/- sekta ya afya

**Na Farida Ramadhani,** DODOMA

TANZANIA na Global Fund zimesaini mikataba minne ya misaada yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 606.9 (Sh. trilioni 1.4) kwa ajili ya kupambana na maradhi ya Ukimwi, kifua kikuu, malaria na uimarishaji wa mifumo ya afya nchini.

Mikataba hiyo imesainiwa jijini Dodoma kati ya Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba na Mkuu wa Global Fund- Afrika, Linden Morrison.

Nchemba alisema msaada huo umepangwa kutekelezwa kwa miaka mitatu na mpaka sasa Tanzania imepokea misaada kwa vipindi vinne Julai 2012 - Disemba 2014, Julai 2015 - Desemba 2017, Januari 2018 - Disemba 2022 na Januari 2021 -Disemba 2023.

"Miradi inayotekelezwa kupitia msaada wa Global Fund kwa kipindi cha kuanzia Januari 2024 hadi Disemba 2026, itatekelezwa na sekta ya umma na binafsi, Wizara ya Fedha inaendelea kuwa mpokeaji mkuu wa sekta ya umma na Management and Development for Health (MDH) ni mpokeaji mkuu wa pili kwa sekta binafsi," alisema Nchemba.

Aidha, aliishukuru kwa kuendelea kuisaidia Tanzania na kubainisha kuwa misaada hiyo inatokana na juhudi mbalimbali anazofanya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameifanya nchi iaminike kimataifa.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema watatumia fedha hizo kikamilifu kuimarisha kinga dhidi ya Ukimwi, malaria na kifua kikuu na asilimia 75 ya fedha hizo zimeelekezwa kwenye bidhaa za afya.

"Kwa upande wa Ukimwi tutahakikisha takribani Watanzania milioni 1.7 ambao wanamaambukizi wanapata dawa za kufubaza makali ya ukimwi (ARV) kila mwaka," alisema Mwalimu.

Alisema, malaria, fedha hizo zitatumika kuiwezesha wizara hiyo kuendelea kutoa huduma bure ya kupima ugonjwa huoa kwa kutumia kipimo cha haraka (MRDT) na kutoa dawa kwa watu milioni 10 kwa kipindi cha miaka mitatu.

"Nasisitiza kwamba kipimo cha malaria cha haraka (MRDT) ni bure, dawa mseto pamoja na sindano ya malaria kali ni bure kwa sababu fedha hizi tulizopata kutoka Global Fund tunakwenda kutumia kununua vifaa vya kupima pamoja na dawa," alisisitiza.

Aliwaagiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya zote nchini kusimamia maelekezo ya serikali ya kuhakikisha huduma hizo zinatolewa bure kwa wananchi.

Alisema kwa upande wa malaria pia watagawa vyandarua vyenye dawa milioni 22.6 kwa makundi mbalimbali hususan wajawazito na watoto walio chini ya miaka mitano.

Mapambano dhidi ya kifua kikuu, alisema watatumia fedha hizo kwa ajili ya kuibua wagonjwa wapya wa ugonjwa huo.

Alisema, fedha hizo pia zitatumika kuimarisha mifumo ya afya na wizara hiyo imepanga kununua vifaatiba kwa ajili ya vituo vya huduma za afya katika ngazi ya kata.

Mkuu wa Global Fund Afrika, Linden Morrison, alisema Tanzania ni nchi ya nne kwa kupata misaada mingi kutoka Mfuko huo pia imekuwa mstari wa mbele katika ukusanyaji na usimamizi wa rasilimali jambo lililosababisha kupewa misaada hiyo.

Alisema msaada uliotolewa ni kwa kipindi cha mwaka 2024 hadi 2026 na inalenga kuboresha mifumo ya maabara, mitungi ya Oksijeni, kuboresha mazingira ya watumishi wa afya na kuimarisha mnyororo wa thamani.

Aidha, alisema msaada huo unakwenda sambamba na vipaumbele vya serikali ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo ya afya nchini.

Ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kufanikisha kusimamia utekelezaji wa programu iliyoishia Disemba 2023 na kupata matokeo mazuri ya matumizi ya fedha kutoka mfuko huo katika masuala yakupunguza maambukizi ya HIV, maralia na kifua kikuu.


**TANGAZO**

**HAFSA BINT AHMED SALIM UNATAFUTWA NA KAKA NA DADA ZAKO**

1. NI MIAKA 49 TANGU UMEZALIWA 1974 HAWAJAKUONA
2. BABA ALIKUONA MWAKA 2006

ULIPOMTEMBELEA NYUMBANI KWAKE SASA NI MIAKA 17.

***FANYA HIMA UWAONE NA KUWAJUA NDUGU ZAKO***

# Neema zaidi ajira 137,294 kutolewa sekta afya

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema itatoa ajira kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii 137,294 kwa kipindi cha miaka mitano, kwenye mradi utakaogharimu Sh. bil. 899.473 ili kupunguza pengo la asilimia 64 la wahudumu hao.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizindua Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii.

Alisema kwa mwaka wa kwanza 2023/2024 serikali itaajiri wahudumu hao 28,000 kwa gharama ya Sh. bilioni 99.78 kwa kuwa kuna mahitaji makubwa katika vituo vya afya ngazi ya msingi.

"Wahudumu hawa watasaidia kutoa huduma afya ya msingi, kinga, afya, uhamishaji wa elimu kulingana na miongozo iliyopo na itakayowekwa.

"Mpango huu unatekelezwa kwa vitendo dhana ya kinga ni bora kuliko tiba na itaipunguzia serikali gharama kubwa za ununuzi wa dawa na kwa mwaka 2023/24 imefikia Sh. bilioni 200," alisema Dk. Mpango.

Alisema pamoja na changamoto za wahudumu bado zipo nyingine katika uratibu na kuathiri shughuli za afya zinazowekwa na serikali na mpango ni kurasimisha wahudumu hao na kuchangia afua jumuishi.

"Ajira hizo kwa upande wa bara na kwa kipindi cha miaka minne mfululizo 27,324 wataajiriwa hadi mwaka 2028 wahudumu hawa watachaguliwa kila kitongoji na mtaa kitakuwa na wahudumu wawili, mwanamke na mwanamume.

"Vitongoji vyote 64,384 na mitaa yote 4,263 ya Tanzania bara, hii ni fursa adhimu na wananchi wote wenye sifa wachangamkie fursa. Wizara na TAMISEMI waangalie mahitaji ya wahudumu wa afya kwa kuendana na idadi ya watu," alisema.

Aidha, wahudumu hao wachaguliwe kwa kuangalia vigezo kwa kuwa watatoa elimu ya afya, huduma tembezi na M-koba, kinga na za awali za tiba, kabla ya kutoa rufani, ingawa kipaumbele ni katika huduma ya mama na mtoto, uzazi wa mpango na vijana, magonjwa ya mlipuko na kuambukiza kama Ukimwi na kifua kikuu.

"Naishukuru Taasisi ya Susan Thompson Buffet Foundation-STBF, walioahidi kutoa mchango kila mwaka katika mpango huu na wadau wengine wa maendeleo. Wizara ya Afya itoe hamasa kwa jamii kurahisisha utekelezaji na wito kwa jamii kuwapatia ushirikiano wa kutosha wahudumu hawa," alisisitiza.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema serikali inajitahidi kuboresha huduma na kugharamia na kwamba wahudumu hao ni muhimu kwa kuwa hivi karibuni walisaidia kugundua waliougua kipindupindu, ikiwamo mkoani Mwanza.

"Tuliweza kugundua mgonjwa wa marburg mkoani Kagera kupitia mhudumu wa ngazi ya jamii. Mpango kama huu umesaidia nchi ya Rwanda kwa asilimia 57 ya kesi zote za malaria kuishia kwa wahudumu wa ngazi ya jamii.

"Wahudumu hawa tulipoamua kuwatumia wamesaidia kuibua wagonjwa wa TB wa zaidi ya asilimia 50 kwa kila wagonjwa 100," alisema Mwalimu.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana (katikati), akifurahia jambo na Balozi wa zamani wa China nchini, Liu Qingyou, walipotembelea kituo cha East Africa Commercial & Logistics Ubungo, Dar es Salaam jana, kuona maendeleo ya ujenzi wa kituo cha biashara. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Spika ataka fedha kutengeneza barabara zilizoathirika na mvua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, ameagiza serikali fedha zinazopelekwa kufungua barabara zilizoathiriwa na mvua, kipaumbele kitolewe kwanza kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano.

Pamoja na maagizo hayo, serikali imesema kabla ya Mkutano wa 14 wa Bunge kumalizika, itatoa Sh. bilioni 30 zilizoombwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kukarabati barabara zilizokumbwa na mafuriko.

Dk. Tulia alitoa agizo hilo jana bungeni baada ya Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Deogratius Ndejembi, kujibu maswali ya wabunge kuhusu maeneo yaliyoathiriwa na mvua inayoendelea kunyesha nchini.

Spika alisema kipaumbele kitolewe kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano kabisa na yafuate yenye mawasiliano lakini hayapitiki na magari yanakwama.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Regina Qwaray, alihoji kuna mpango gani wa dharura wa kuzikarabati barabara za vijijini katika mkoa wa Manyara zilizoharibiwa na mvua ya el- Nino.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ndejembi alisema serikali imeshaanza kuzikarabati barabara za vijijini zilizoharibiwa na mvua na Sh. milioni 498 zimepelekwa TARURA Mkoa wa Manyara kwa ajili ya kurekebisha uharibifu unaoweza kufanywa kwa sasa ikiwamo kuondoa tope barabarani, kuchonga baadhi ya barabara, kuweka changarawe, kuchimba na kusafisha mifereji na kurekebisha mikondo ya mito.

Alisisitiza serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha za kurekebisha miundombinu ya barabara ziliyoathiriwa na mvua zinazoendelea kunyesha kote nchini.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Kawe (CCM), Josephat Gwajima, alisema barabara za jimbo hilo zote zimevunjika na kutoka vipande vipande kwasababu ya wingi wa mvua zinazonyesha na kuhoji mpango wa dharura wa serikali kuokoa barabara hizo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ndejembi alisema fedha ya dharura imeanza kwenda kwenye maeneo mbalimbali nchini na kwa Kawe zimepelekwa Sh.Milioni 598 ili kuanza kufungua barabara na kuanza kupitika.

"Fedha nyingine Sh. bilioni 30 tunasubiri wenzetu wa Wizara ya Fedha ili kuendelea kufungua barabara maeneo mengine nchini," alisema.

Akitolea ufafanuzi fedha hizo zilizoombwa na TAMISEMI, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, aliahidi kabla mkutano huo wa bunge, Hazina itatoa fedha hizo ili kurejesha miundombinu.

## Watoto wafa maji wakitoka twisheni

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Msingi Tumaini, Kata ya Karanga, Manispaa ya Moshi, wanadaiwa kupoteza maisha baada ya kuchukuliwa na maji wakati wakiogelea Mto Karanga.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Bonite, Peter William, alisema Januari 27, majira ya jioni, alipata taarifa ya kuwapo kwa tukio la wanafunzi wawili wa shule hiyo waliotumbukia mtoni baada ya kutoka shuleni kwenye masomo ya ziada.

"Nilifika eneo hilo na kupata taarifa kutoka kwa walimu na baadhi ya wananchi wakiwatafuta watoto hao ambao inadaiwa walifika eneo hilo kwa ajili ya kuogelea," alisema.

Naye mzazi wa mmoja wa watoto waliopotea, Dismas Kimati, alisema mwanawe aliondoka asubuhi kwa ajili ya kwenda shuleni kwa ajili ya masomo ya ziada na majira ya saa 8:00 mchana, alipata taarifa kutoka kwa mkewe kwa kutofika kwa mwanawe licha ya watoto wa jirani kufika.

"Mke wangu ambaye ni mzazi alinipigia simu akinielezea kutofika kwa mwanangu jambo ambalo si kawaida yake. Nilipatwa na wasiwasi na kwenda shuleni ambako nilikutana na mwalimu akaniambia watoto wametoka shuleni toka saa 8:00 mchana. Nikaenda kwa marafiki zake ninaowafahamu mmoja akanijuza kuwa walielekea mtoni.

"Nilipofika eneo la mto nikakutana na viongozi wa mtaa na baadhi ya wananchi wakiwa tayari wamepata taarifa hizo na kuanza kuwatafuta hadi majira ya usiku wa saa 6:00 sita tukaona begi," alisema.

Akidhibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, alisema Januari 29, mwaka huu, majira 11:45 maeneo Chekereni, Kata ya Kindi, Wilaya ya Moshi, mwanafunzi wa darasa la saba wa Shule ya Msingi Tumaini, Rodrick Orota (14), alikutwa amefariki dunia ndani ya Mto Karanga baada ya kupotea toka Januari 27, mwaka huu.

Kamanda alisema mtoto huyo alitoweka baada ya kutoka shuleni Jumamosi kwenye masomo ya ziada akiwa rafiki yake, Ridhiwani Kimath, ambaye hajapatikana.

"Pembeni mwa mto zilikutwa nguo zao. Inaonekana waliingia mtoni kwa ajili ya kuogelea, jitihada za kumtafuta Ridhiwani zinaendelea na mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi kwa ajili ya uchunguzi wa daktari," alisema.

TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mipango kuendeleza sekta ya uvuvi itekelezwe kwa vitendo

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi alizindua ugawaji wa vizimba vya ufugaji wa samaki na boti za kisasa kwa wavuvi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa huku akibainisha mambo 10 yanayoendelea katika kuimarisha sekta hiyo na hatimaye kuchangia pato la taifa kwa asilimia 10 kutoka asilimia 1.8 ya sasa ifikapo mwaka 2030.

Pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali katika mipango mbalimbali inayohusisha maendeleo na mageuzi katika sekta hiyo, Rais Samia alionyesha kutokuridhishwa na pato linalopatikana kutokana na sekta hiyo. Kutokana na hali hiyo, alisema serikali yake imedhamiria kufanya mageuzi ya kweli kwa kuongeza mauzo ya mazao ya samaki ndani na nje.

Tanzania ina hazina kubwa ya Bahari ya Hindi, maziwa, mito na mabwawa ambayo yakitumika ipasavyo yanaweza kuleta matokeo chanya katika sekta ya uvuvi. Mbali na Bahari ya Hindi kutoka Tanga hadi Mtwara, Tanzania pia ina maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa na Rukwa na mabwawa kadhaa likiwamo la Mtera ambayo kwa hakika yana samaki wengi.

Kwa kutambua hilo, Rais Samia alitaja baadhi ya mambo yanayofanywa katika kuleta mageuzi kwenye sekta hiyo kuwa ni kuimarisha utendaji kazi katika sekta ikiwamo wizara yenye dhamana, kuweka miundo ya wawekezaji kibiashara kutoka ndani na nje, kuanzisha wakala wa kusimamia maendeleo ya uvuvi, kutatua changamoto zinazowakabili wavuvi na kutoa ajira kwa vijana kupitia uvuvi.

Mipango mingine ni kutoa zana za kisasa za uvuvi, ufugaji samaki kwa makundi mbalimbali wakiwamo vijana na wanawake, ujenzi wa bandari kubwa za uvuvi katika ukanda wa Afrika Mashariki zinazoendelea kujengwa Kilwa na Bagamoyo, na kujenga miundombinu ya usafirishaji ikiwamo barabara, viwanja vya ndege hasa wa Mwanza ambao utakuwa ukisafirisha mazao hayo na maeneo ya kuhifadhia.

Pia Rais alitaja mpango wa ununuzi wa meli za kisasa za uvuvi, ujenzi wa vituo vya kuendeleza ufugaji wa viumbe maji, mashamba darasa ya ufugaji wa uvuvi pamoja kuongeza bajeti katika Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi sambamba na kuongeza uwekezaji katika sekta hiyo.

Takwimu zilizotolewa kuhusu mchango wa sekta ya uvuvi ni mdogo sana kulinganisha na rasilimali zilizoko nchini ndiyo maana Rais na serikali yake ameamua kuchukua hatua madhubuti katika kuendeleza sekta hiyo na kutoa mchango na maendeleo chanya kwa uchumi wa taifa. Kwa hakika hatua hiyo ni ya kupongewa.


Iko mipango mingi ambayo imekuwa ikibuniwa na serikali katika kukuza uchumi wa nchi na kupambana na umaskini lakini imekuwa ikiishia njiani. Baadhi ya mipango hiyo ni Kilimo Kwanza na Matokeo Makubwa Sasa (BRN), hivyo kama wahenga wasemavyo ukiumwa na nyoka hata ukiona unyasi utashtuka, tahadhari inapaswa kuchukuliwa katika kutekeleza mipango hiyo na kuleta matokeo makubwa.

Ni wazi kwamba nia ya Rais ni nzuri lakini watekelezaji ndio wamekuwa tatizo. Hilo linajidhihirisha kupitia mipango iliyobuniwa awali lakini haikuleta matokeo tarajiwa. Kwa hiyo somo litokane na historia na hatimaye kwenda kwenye matokeo chanya ya sekta ya uvuvi.

Kama ilivyoelezwa awali, Tanzania ina rasilimali nyingi za uvuvi ambazo kama zitatumika ipasavyo kwa maendeleo ya sekta ikiwamo uwekezaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya samaki, hatua kubwa itapigwa na taifa litapiga hatua kubwa katika maendeleo.

Utashi wa kisiasa katika maendeleo ya sekta ya uvuvi umeonekana dhahiri baada ya Rais Samia kueleza mipango kabambe iliyowekwa katika eneo hilo. Sasa ni wajibu wa watendaji kuchukua hatua na kutekeleza ili kukuza uchumi wa nchi na kutatua changamoto ya ajira kwa vijana kupitia uvuvi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kulikoni ahadi za maji, umeme kurejea zinakinzana na uhalisia?

Na Beatrice Moses

**MALALAMIKO** ya kukatika umeme kila mara, maji na kupanda kwa bei na kuadimika kwa sukari yanayotoka kwa wananchi kwa hakika yanaumiza, hasa kwa kuwa vitu hivyo vyote ni muhimu kwa jamii.

Kuna matamko kadhaa ambayo yametolewa na baadhi ya viongozi kuhusu kero hizo, pamoja na ahadi nzuri kwamba hali hiyo iwe ya kukatika umeme, uhaba wa maji ni wa muda na inatafutiwa ufumbuzi, lakini wahenga wanasema "maneno matupu hayavunji mfupa".

Mnamo Desemba 20, 2023, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, akatoa ahadi kuwa tatizo la mgao wa umeme litakwisha ifikapo Januari mwaka 2024, baada ya mtambo mmoja wa kuzalisha umeme kutoka bwawa la Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP) kuanza majaribio ya kuzalisha umeme utakaoingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

Mhandisi Mramba aliyasema hayo, wakati akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kukagua kiwango cha maji katika chanzo cha kuzalisha umeme cha bwawa la Mtera lililopo wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma.

Akasema kwamba, umeme utakaoingizwa ni megawati 235 zitakazosaidia kupunguza makali ya mgao, kwa kuwa upungufu uliopo nchini ni kati ya megawati 250 hadi 300.

Pia akazungumzia kina cha maji cha bwawa la Mtera kutofikia kiwango kinachotakiwa cha mita 691, walitegemea kina cha maji katika bwawa hilo kitaongezeka kuanzia Desemba 25 hadi 26 mwaka mwaka 2023, baada ya Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) kuwathibitishia kutakuwa na mvua za kutosha kwenye mikoa ya Iringa na Mbeya ambayo maji yake yanaingia kwenye bwawa hilo.

"Niwatoe hofu wananchi kuhusu mgao wa umeme kuwa utaisha ndani ya wiki tatu za kwanza za mwezi Januari mwaka 2024, kwa sababu pamoja na mvua kunyesha kwenye mikoa hiyo.

"Pia tutaingiza megawati 235 kwa majaribio ya mtambo mmoja kutoka bwawa la Mwalimu Julius Nyerere kwenye gridi ya Taifa," alikaririwa akizungumza Mhandisi Mramba.

Katibu Mkuu anasema kuwa, upungufu wa umeme nchini utakuwa historia kwa kuwa mwezi Machi 2024 zitaingizwa tena megawati 235 na kufanya jumla ya megawati 470, baada ya mtambo wa pili kuanza kufanya kazi, hivyo kuondoa uhitaji wa megawati 300 ambazo ndizo upungufu uliopo kwa sasa.

Hiyo ni mojawapo ya ahadi kubwa ambayo ilitolewa na wananchi wakaipokea kwa matumaini, sasa ni Februari imeingia na bado kuna tatizo la kukatwa kwa umeme, wakati mwingine hata bila ya taarifa, jambo ambalo linawakera wananchi wengi.

Umeme ni huduma muhimu, pia tayari imeshalipiwa, hivyo mwananchi anapaswa kuitumia tu kwa kadri alivyolipia, sasa kukatwa kwa umeme mara kwa mara, kunasababisha hasara na usumbufu wa aina yake kwa jamii.

Kwenye makundi kadhaa niliyopo, nimeshuhudia ujumbe wa malalamiko kutoka kwa wanavikundi kuhusu kukosekana kwa huduma hiyo pamoja na maji.

Wengi wanahoji inakuwaje huduma hizi muhimu zinakosekana wakati huu, ambao mvua zinanyesha kubwa kiasi cha kusababibisha mafuriko?

Wapo wanaolalamika kukosa maji kwa muda wa takribani wiki tatu, mvua zinazonyesha ndiyo zimewapa unafuu kiasi fulani kwa kuwa wapo ambao wamechimba visima, hivyo wanaambulia maji hayo ya mvua.

Japo ni wazi kuwa hakuna uhakika wa usalama wake kwa kuwa katika kipindi hiki, pia baadhi ya chemba za majitaka hutobolewa ama kufurika zenyewe, huku tayari kukiwa na taarifa za kuibuka ugonjwa wa kipindupindu.

Wakati kuna mgao wa kupata huduma hizo muhimu katika baadhi ya maeneo, pia kuna kilio cha kupanda kwa bei ya sukari kiasi cha kufikia kuuzwa Sh. 5,000 kwa kilo moja.

Sukari ni miongoni mwa bidhaa muhimu kwa matumizi ya mlo na kiburudisho kwenye familia, ukiacha kwa wale ambao wamezuiliwa kuitumia kutokana na kuwa na magonjwa yasiyoruhusiwa matumizi ya sukari.

Viongozi wanaohusika ni vyema wajitafakari kutokana na kukithiri kwa kero hizo na matamko yasiyo na majibu ya uhakika. Wananchi wanatamani kuona huduma hizo zinakuwa za uhakika, ili waendelee na shughuli zao kwa utulivu.

# Madaktari wazawa watenganisha watoto waliozaliwa wameungana

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imeweka rekodi kwa kufanya upasuaji mkubwa wa kuwatenganisha pacha walioungana sehemu ya tumbo na kifua.

Huo ni upasuaji wa kwanza kufanywa na madaktari wazawa hapa nchini, umefanyika kwa saa sita, ni wa kwanza kufanywa na madaktari wazawa na kuwa upasuaji wa nne wa aina hiyo kufanyika MNH.

Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji MNH, Dk. Rachel Mhaville, alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam kwamba upasuaji huo umefanikiwa kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali kwa kununua vifaa tiba vya kisasa pamoja na kuwasomesha wataalamu.

"Tunachojivunia katika upasuaji huu ni kuwa umefanywa na timu ya madaktari wazawa, umefanyika kwa mafanikio makubwa na watoto wanaendelea vizuri kabisa. "Pamoja na kufanikiwa kufanya upasuaji huu, bado tutaendelea kushirikiana na wataalamu wengine kuendelea kupata ujuzi zaidi na kuendeleza uhusiano," alisisitiza Dk. Mhavile.

Bingwa wa Upasuaji wa Watoto MNH, Dk. Victor Ngota, alisema upasuaji wa kuwatenganisha watoto unahitaji utaalamu wa hali ya juu, hivyo ulihusisha jopo la wataalamu mbalimbali wakiwamo madaktari bingwa wa upasuaji watoto, upasuaji rekebishi, wataalamu wa usingizi, wataalamu wa lishe na radiolojia.

"Tuliwapokea watoto hawa Machi 11, 2023 hivyo tulianza mchakato wa kuwahusisha wataalamu ambao wanahusika na huduma hizi, ilituchukua takribani muda wa miezi 10 kuangalia mwenendo wao wa afya kwa ujumla kabla ya kuwatenganisha, ili kuweza kupata dira ya namna watakavyoishi baada ya kutenganishwa," alisema Dk. Ngota.




Baadhi ya wafanyabiashara wakiwa wamefungua maduka yao ndani ya kituo kipya cha mabasi cha Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana. **PICHA: JENIFER GILLA**

## Maduka ya biashara Mwenge yaanza kazi

**Na Jenifer Gilla**

BAADA ya ukimya wa muda mrefu, hatimaye maduka ya biashara katika kituo cha mabasi cha Mwenge, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, yameanza kufunguliwa na wafanyabiashara waliokodishwa wameanza kuhamia rasmi katika eneo hilo.

Nipashe ilitembelea eneo hilo na kukuta baadhi ya vibanda vikiwa vimefunguliwa na vingine wamiliki wake wakiendelea kufanya maboresho kulingana na aina ya biashara wanazotaka kuweka.

Ofisa Uwekezaji wa Manispaa ya Kinondoni, Shadrak Mbuni, aliiambia Nipashe kuwa walishakabidhi maduka hayo kwa wafanyabiashara na walianza kufungua tangu Januari 20, mwaka huu.

"Kuna fremu kama 20 mpaka sasa zimeanza kufanya kazi, kuna wanaouza sola, wanaouza chakula. Wengine wanarekebisha ndani kwa ajili ya kuweka biashara zao, wakimaliza utawaona na wao wanahamia," alisema.

Kuhusu kituo cha mabasi ya abiria, Mbuni alisema tayari kimeshaanza kutumiwa kwa mabasi ya abiria, maarufu kama daladala kupita kwa ajili ya kushusha na kupakia abiria.

Wakati huo huo, Baraza la Madiwani la Manispaa ya Kinondoni juzi lilifanya kikao cha kupitisha bajeti ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 ya Sh. bilioni 149.45.

Akizungumza katika kikao hicho, Meya wa Manispaa hiyo, Songoro Mnyonge, alisema katika fedha hizo, Sh. bilioni 74.2 zinatokana na makusanyo ya ndani na Sh. bilioni 75.2 ni ruzuku kutoka serikalini.

Alisema katika fedha za makusanyo ya ndani wametenga Sh.bilioni 42 .27 sawa na asilimia 70 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni agizo la serikali.

Alisema katika bajeti kwa ujumla kuna miradi ambayo itapewa kipaumbele ikiwamo uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Oktoba mwaka huu ambao wameutengea Sh. milioni 500.

"Ingawa mipango ya uchaguzi inasimamiwa na TAMISEMI (Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) sisi tukasema tujiongeze pale ambapo itachelewa kuleta fedha angalau na sisi tuwe na pa kuanzia," alisema.

Alitaja eneo lingine wanalolipa kipaumbele katika bajeti hiyo ni mfuko wa vijana, wanawake na wenye ulemavu ambao wameutengea Sh. bilioni 6.039 kwa ajili ya kuliinua kundi hilo kiuchumi kupitia mikopo.

Mnyonge alisema pia wametenga Sh.bilioni 6.039 kwa ajili ya kuusaidia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kuboresha miundombinu ya barabara katika manispaa hiyo.

Alisema baada ya kikao hicho bajeti hiyo itapelekwa bungeni kwa ajili ya kupitishwa na wabunge na ikifanikiwa itaanza kutumika rasmi Julai 2024.

Alimpongeza Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Hanifa Hamza, kwa kazi kubwa anayoifanya kukusanya mapato hayo na kupunguzia serikali mzigo wa kutoa fedha za ruzuku.

Alimhimiza kuendelea na kasi hiyo ya makusanyo ili utekelezaji wa miradi katika bajeti ya sasa upite ule wa mwaka uliopita ambao ulikuwa ni asilimia 91.

Meya Songoro aliwasihi pia watumishi wa manispaa hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kutekeleza miradi iliyoazimiwa katika bajeti ya mwaka wa fedha uliopo 2023/24 kabla ya kufikia mwaka ujao wa fedha.

# Madereva wafurahi kuondolewa foleni mizani barabarani

**Na Idda Mushi,** KILOSA

MADEREVA wa magari makubwa wanaotumia barabara ya Mikumi-Iringa, wilayani Kilosa, mkoani Morogoro wamepongeza hatua ya serikali kuboresha miundombinu ya mizani na kuondoa foleni iliyosababisha kupoteza muda mrefu eneo hilo.

Mwandishi wa habari hii aliyefika eneo la Mikumi alishuhudia magari makubwa yakipita bila kuingia kwenye mizani, kutokana na kupima kisasa yakiwa yanatembea na yenye shaka na uzito yakiingia kupima bila kuwapo foleni tofauti na awali.

Baadhi ya madereva waliokutwa wakipima, Nicholas Kweka na Shomari Mgoa, walisema hali ya sasa ya mizani imerahisisha safari zao kwa kuwa awali walikuwa wakitumia muda mrefu mizani kupima na kuchelewesha bidhaa wanazosafirisha na kushindwa kufika kwa wakati kuendelea na majukumu mengine.

"Hali mwanzo ilikuwa mbaya tulitumia muda mrefu katika eneo hili la mizani, lakini sasa hivi hali ni nzuri kwa sababu sensa zimeondoa msongamano, ukipita kwenye spidi stahiki na kuacha nafasi kwa gari ya mbele yako basi inakuruhusu kupita, hii imerahisisha shughuli zetu kwa kiasi kikubwa kwa sababu plan (mipango) ya safari ulivyopanga inakwenda kama inavyopaswa kuwa, kikubwa ni watumishi kufanya kazi kwa uadilifu," alisema Mgoa.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, alisema serikali itaendelea kuboresha mizani kuwa za kisasa zaidi kwa kuwezesha kuwa na pande mbili ili magari yanayokwenda na kurudi yote yapime kwa wakati na pia kuwezesha kupima bila kusimama.

"Mizani inajengwa na serikali na mkandarasi anapewa kazi ya kufanya kwa maelekezo, sehemu kubwa ambayo tumefanya, tuna mizani ambayo ni 'way in motion', yani mizani ambayo magari yanatembea huku yanapima, inasaidia, lakini pia kuwa na mizani pande mbili ambayo magari yakitoka huko hayalazimiki kwenda upande mwingine, gari hazisimami na magari yasiyo na uzito mkubwa hayalazimiki kupima, yanapita tu," alisema Naibu waziri.

Alisema nia ni kujenga mizani za aina hiyo maeneo yote nchini hasa yanayopitisha magari mengi makubwa na kwenye msongamano ili kurahisisha upimaji na kuondoa foleni maeneo ya mizani. "Ukiangalia hizi barabara kubwa, wenzetu wanaotoka nchi za nje, moja ya kitu ambacho ni kero kwao ni kuwa na mizani nyingi na zinazochukua muda, ndio maana tumeamua tuanze na hiyo kuhakikisha tumeondoa mizani ya zamani na kuweka ya kisasa ambayo gari itapima huku inatembea na kupunguza muda wa kukaa muda mrefu," alisema.

Aidha, alisema mizani hizo hazitakuwa Mikumi pekee, zitakuwa maeneo mengine ikiwamo Makambako,Tunduma, Nyakanazi yenye msongamano wa magari.

"Wingi wa magari unaonesha nchi inafunguka, sasa kwa mazingira hayo ndio maana wizara ya ujenzi tunaongeza mizani na kuboresha kuwa ya kisasa ili kuondoa foleni nchi nzima, hasa kwenye barabara kubwa," alisema.

Alisema mizani hizo zimefungwa kamera za kisasa na mfumo wa taarifa, gari ikipima zinaonekana kwenye mamlaka mbalimbali, hali inayoondoa uwezekano wa kushawishi rushwa na kubadili taarifa zozote.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoani Morogoro, Mhandisi Alinanuswe Kyamba, alisema wamefanikisha maboresho ya mzani huo na kuufanya kuwa wa kisasa ili kusaidia kuondoa vichocheo vya rushwa na kuondoa foleni kubwa iliyokuwepo awali.

Mhandisi Kyamba alisema mizani hiyo imejengwa pande zote mbili za barabara ikiwa na viashiria au sensa kudhibiti uzito wa magari, ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni 1.9.

# Biashara Tanzania, Misri yafikia Dola milioni 6.3

**Na Joseph Mwendapole**

BIASHARA kati ya Tanzania na Misri imeendelea kuongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 4.9 mwaka 2018 hadi kufikia Dola milioni 6.3 mwaka 2022.

Pamoja na kuongezeka kwa biashara baina ya mataifa hayo, imeelezwa kuwa bado kuna fursa nyingi za biashara ambazo wananchi wanapaswa kuzichangamkia.

Hayo yalisemwa jana na Meneja wa Uendelezaji Biashara wa Mamlaka ya Kuendeleza Biashara (Tantrade), Mohamed Tajiri, wakati wa mjadala wa uwekezaji baina ya wafanyabiashara wa Misri na Tanzania, ulioandaliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Alisema kwa miaka mingi Tanzania imeendelea kuuza Misri kahawa, tumbaku, samaki na mbegu za mafuta wakati ikiagiza kutoka nchi hiyo chuma, vifaa vya umeme, dawa, vifaa tiba, sukari, plastiki, samani za ndani na vifaa vya ujenzi.

"Ingawa tunafanya biashara nzuri na Misri, bado kuna fursa nyingi za uwekezaji baina ya wafanyabiashara wa mataifa haya. Kwa mfano bado bidhaa za Tanzania zina soko kubwa Misri, kwa hiyo wafanyabiashara wetu wanapaswa kuiona hiyo fursa," alisema.

Akizungumza wakati akifungua mjadala huo, Mkuu wa Idara ya Uchumi na Biashara Ubalozi wa Misri, Mohamed Atteya, alisema mkutano huo ni muhimu kwa ustawi wa biashara baina ya mataifa hayo mawili.

Alisema mkutano huo utatoa fursa ya kuchangamana kwa wafanyabiashara wa mataifa hayo ambapo watabadilishana fursa zinazopatikana kwenye mataifa hayo.

"Siku zote huwa tunakaribisha matukio kama haya na tunaona fahari kuwa na mikutano kama hii kwasababu inatuwezesha kuwaunganisha watu wa sekta binafsi kwa mataifa yetu mawili hasa kwenye eneo la uwekezaji na biashara.

"Naona fahari kusema kwamba kiwango cha biashara baina ya mataifa haya mawili imeongezeka kwa asilimia 45 kwa mwaka 2022 na kwa mujibu wa taarifa za Kituo cha Uwekezaji TIC uwekezaji wa Misri nchini Tanzania umeongezeka na kufikia Dola za Marekani bilioni 1.3," alisema.

Pia alisema anasikia fahari kuona kwamba kampuni mbili za Misri zinashirikiana na serikali ya Tanzania kujenga bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere Rufiji ambalo kukamilika kwake kutasaidia nchi kuwa na umeme wa uhakika na kusaidia ukuaji wa uchumi," alisema.

Ofisa Uwekezaji wa TIC, Diana Mwamanga, alisema lengo la mkutano huo ni kuwaeleza wafanyabiashara wa Misri fursa zilizoko Tanzania na wale wa nchi hiyo kuwaeleza wenzao wa Tanzania wanachoweza kuuza hapa nchini.

"Kwenye mkutano huu wafanyabiashara wa Misri wameonyesha nia ya kuwekeza kwenye sekta ya afya, sekta ya ujenzi, dawa za binadamu, nguo na tumewafahamisha kuhusu sekta zingine ambazo wanaweza kuwekeza," alisema.




Waziri wa Fedha na Uchumi Zanzibar, Dk. Saada Mkuya (wa pili kushoto), akitoa zawadi maalumu kwa Mkuu wa Idara ya Islamic Banking wa Benki ya KCB Tanzania, Amour Muro kwa ajili ya utekelezaji na ushiriki wa benki hiyo katika uzinduzi wa First United Takaful, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: HISANI YA KCB**

# Bandari Dar yapokea meli kubwa ya mizigo

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Profesa Godius Kahyarara, amesema Bandari ya Dar es Salaam ipo tayari kupokea meli kubwa za mizigo kutoka mataifa mbalimbali kutokana na maboresho yaliyofanyika ambayo yameongeza ufanisi katika kuhudumia shehena za mizigo.

Aliyasema hayo juzi baada ya kupokea meli ya mizigo ya Shirika la KMTC kutoka China, inayofanya safari zake moja kwa moja kutoka nchini humo hadi Tanzania ikiwa na makasha 1,500.

"Tunajivunia sana kazi inayofanyika hapa, tunaona mabadiliko makubwa kwa kuwa tumepokea meli iliyotoka China moja kwa moja. Uwezo wetu kuhudumia shehena ni mkubwa na wenye ufanisi mzuri," alisema.

Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mrisho Mrisho alisema kutokana na maboresho yaliyofanyika bandarini hapo, sasa inahudumia shehena kubwa ya mizigo kutokana na wingi wa meli zinazotia nanga kila siku.

Bandari ya Dar es Salaam inakuwa ya kwanza Afrika kwa meli ya Shirika la KMTC kutia nanga ikiwa imebeba mzigo wa makasha 1,500.

KMTC (Korea Marine Transport Co. Lts) ilianzishwa mwaka 1954 ikiwa ni kampuni kiongozi katika ubebaji mizigo kwa usafiri wa majini kutoka bara moja hadi jingine.

"Kwa miaka 60 tumekuwa watoa huduma bora kati ya Asia na masoko ya India pamoja na ukanda wa Afrika Mashariki na Afrika ya Kati. Mwaka 2022 KMTC ilikuwa ni kampuni namba moja ikiwa na hisa Korea, Japan na Kusini mwa Asia ikiunganisha bandari za kimataifa 90 katika nchi 25," ilifafanua taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo.

## Pinda awafunda watendaji ardhi

**Na Munir Shemweta,** MWANZA

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amewafunda watendaji wa ardhi katika Jiji la Mwanza kwa kuwataka kusimamia sekta hiyo kwa kuzingatia kanuni, taratibu na miongozo.

Amesema kwa kufanya hivyo, wizara itaepukana na migogoro ya ardhi isiyo ya lazima aliyoieleza kuwa imeendelea kuibuka kila kukicha katika maeneo mbalimbali.

Pinda alisema hayo juzi alipokutana na wakuu wa idara na vitengo wanaosimamia sekta ya ardhi katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza pamoja na wale wa Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mwanza akiwa katika ziara yake mkoani hapa.

"Ninyi ndio wasimamizi wa sekta hii ya ardhi katika jiji la Mwanza, hivyo mna wajibu mkubwa wa kufuata kanuni, taratibu na miongozo ili kuepusha migogoro ya ardhi," alisema.

Amewataka wakuu hao wa idara na vitengo kuwa washauri wazuri wa wakurugenzi wa halmashauri ikiwamo kuzishauri halmashauri kuwa na benki za ardhi katika maeneo yao.

"Ninachotaka kuwaambia silka yangu ni kuwapitisha katika maeneo mnayoyasimamia na hii itawasaidia kutekeleza majukumu yenu kwa ufasaha," alisisitiza.

Aidha, Naibu Waziri Pinda alihimiza upendo miongoni mwa watumishi wakati wote wa utendaji kazi kwa kuwa ndiyo njia pekee ya kuwawezesha kufanya kazi bila kulaumiwa.

Pia aliwataka wakuu wa idara na vitengo katika sekta ya ardhi kuwa na mipango madhubuti itakayofanikisha kuzuia ujenzi holela pamoja na kuhakikisha maeneo ya wazi yanalindwa.

Aliwataka watendaji hao kuhakikisha wanatatua migogoro ya ardhi katika maeneo yao kwa busara ikiwamo kufanya vikao vya kumaliza tofauti kwa amani.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mwanza, Happiness Mtutwa, alimshukuru Naibu Waziri kwa kuwafunda na kuwapa elimu na maelekezo na kusema hilo ni jambo muhimu sana katika kuiboresha sekta ya ardhi.

Alisema wamepokea maelekezo na namna ya kuyashusha kwa watumishi wa chini ili hatimaye maeneo wanayoyasimamia yawe salama.

"Nikutoe hofu Mheshimiwa Waziri ofisi ni taasisi na mara nyingi tumekuwa tukifanyia maelekezo tunayopatiwa na nikuahidi kutekeleza maelekezo na ushauri ulioutoa kwetu kwa kuwa ndiyo msingi wa kuiboresha sekta ya ardhi nchini," alisema Mtutwa.



# Kifua kikuu bado tishio Manyara

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

UGONJWA wa kifua kikuu (TB) umeendelea kuwa tishio katika Mkoa wa Manyara baada ya kugundulika kuwa na maambukizi kwa watu 3,992 katika kipindi cha mwaka jana, imefahamika.

Mratibu wa TB na Ukoma wa mkoa huo, Dk. Mandala Adam, aliliambia Nipashe katika mahojiano maalumu kuhusiana hali ya ugonjwa huo katika kipindi hicho cha kuanzia Januari hadi Desemba mwaka jana.

Dk. Adam alisema Manyara ilikuwa na lengo la kugundua wagonjwa 3,688 kwa mwaka huo badala yake wamebaini kuwa wameongezeka hadi kufikia 3,992.

Alisema kati ya hao watoto wa mwaka sifuri mpaka minne ni 332 huku wanawake wakiwa 2,003.

Awali Mratibu huyo, alisema mwaka 2020, Manyara ilikuwa ni miongoni mwa mikoa mitano yenye idadi kubwa ya wagonjwa wa TB nchini na kwa mwaka jana mikoa 10.

Alisema TB inashambulia mapafu na chanzo ni bakteria ambaye haonekani kwa macho, baadhi ya dalili kukohoa kwa wiki mbili au zaidi, kutokwa jasho usiku na kwa watoto kupungua uzito au kuwa na lishe duni.

Alisema mtoto anapata TB kutoka kwa mtu mzima na wanapozaliwa kinga inakuwa haijakomaa.

Alizitaja njia za kuzuia maambukizi ya TB kwa watoto kuwa ni kuwapatia chanjo baada ya kuzaliwa wakiwa na siku sifuri na wale wanaoishi na wagonjwa kupewa tiba kinga.

"Mtoto kulialia na kukosa hamu ya chakula na uvimbe kwenye shingo ni viashiria vya kuwa na TB," alisema.

Alisema ili kubaini ugonjwa huo kwa watoto, wakifikishwa hospitalini wanachukuliwa makohozi au haja kubwa kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi.

"TB inaweza kumpata kila mtu awe mtoto au mtu mzima ila watoto, wajawazito, wazee, wagonjwa wa sukari, wenye VVU (Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi) na wanaoishi kwenye msongamano," alisema Dk. Adam.

Alifafanua kuwa katika miaka ya nyuma, matibabu ya TB ilikuwa ni kwa mgonjwa kutumia dawa kwa miaka miwili, kwa sasa ni miezi sita kwa dawa mseto nne.

Alifafanua kuwa, dawa ya kwanza ni kwa miezi miwili na ya pili kwa minne ya mwisho, hivyo kukamilisha siku 168 sawa na kipindi hicho cha miezi sita.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2021, watoto milioni 1.2 walibainika kuendelea kuwa na TB, kati ya hao, asilimia 14 walipoteza maisha kwa ugonjwa huo.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa TB inasababisha vifo vya watoto zaidi ya 70,000 kila mwaka duniani.

## REA yaagizwa kupeleka umeme Ngorongoro vijijini

**Na Allan Isack,** LONGIDO

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, amemwagiza Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kupeleka umeme kwenye vijiji saba vilivyopo wilayani Ngorongoro.

Mongela alitoa agizo hilo jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Kitumbeine ikiwa ni ziara yake ya kukagua utekelezaji wa miradi ya afya na elimu wilayani Longido.


"Katika mkoa wetu wa Arusha vijiji karibia vyote vimefikiwa na umeme isipokuwa vijiji saba vilivyoko wilayani Ngorongoro na mpango wa serikali chini ya uongozi wa Rais Samia baada ya kukamilika kwa kazi ya kupeleka umeme vijijini nguvu itaelekezwa kwa vitongoji vyote kuhakikisha vinafikiwa na huduma ya nishati ya umeme," alisema Mongela.

Mkuu huyo wa mkoa, alimwagiza REA kukamilisha mchakato wa kufikisha umeme kwenye vijiji hivyo vilivyosalia, shule, zahanati na vituo vya afya.

Lucas Laizer, mkazi wa Kijiji cha Lopoloisee Kata ya Kitumbeine, akizungumza kwenye mkutano huo, alimuomba Mongela kumwagiza REA kupeleka umeme katika Shule ya Msingi Mangula na Kituo cha Afya Kitumbeine.

Alisema endapo nishati hiyo itafikishwa shuleni kutawasaidia wanafunzi kujisomea na kwenye kituo hicho cha afya, kutarahisisha utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi.

**Lucas Laizer, mkazi wa Kijiji cha Lopoloisee Kata ya Kitumbeine, akizungumza kwenye mkutano huo, alimuomba Mongela kumwagiza REA kupeleka umeme katika Shule ya Msingi Mangula na Kituo cha Afya Kitumbeine.**



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, akisalimiana na mtoto wa wafugaji ambaye familia yao imehamia kwa hiari katika Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni, kutokea Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, mkoani Arusha, alipotembelea kijijini hapo juzi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Watakiwa kujitokeza kuchukua Vitambulisho vya NIDA

**Na Steven William,**
MUHEZA

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imezindua ugawaji wa vitambulisho wilayani hapa Mkoa wa Tanga na kuwataka wananchi kujitokeza kuchukua na kuvitumia kupata huduma muhimu katika jamii.

Uzinduzi huo kiwilaya ulifanyika mapema wiki hii katika Ofisi ya Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kwamkabara.

Akizindua ugawaji huo, Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha wananchi wilayani hapa wanapata vitambulisho vya NIDA.

"Naomba nichukue fursa hii kukupongeza sana Rais Samia, Mkurugenzi Mkuu, Menejimenti na wafanyakazi wote wa NIDA kwa jitihada hizi zinazoleta tija kwa maslahi ya taifa, endeleeni na kasi hii ili muweze kufikia malengo mliyojiwekea ndani ya muda ili tatizo hili tuondokane nalo kabisa," alisema Mfaki.

Aliwataka viongozi kushirikiana kufanikisha ugawaji wa vitambulisho hivyo kwa wananchi wilayani hapa.

"Nitoe rai kwa wananchi wilayani Muheza kujitokeza kwa wingi kuchukua vitambulisho vyao kwenye ofisi za kata na za serikali za mitaa," alisema.

Mfaki aliwahakikisha wananchi hao kuwa serikali imedhamiria kuondoa changamoto ya upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa kwa kuwa vinatolewa bure.


Aliwakumbusha kuvitunza na kuvitumia kwa ajili ya kupata huduma muhimu kama vile kujiunga na bima ya afya, kufungua kampuni, biashara, kupata ajira na mikopo kwenye taasisi za fedha nchini na mikopo ya elimu ya juu.

Katibu Tawala huyo, alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha wazazi na walezi kutunza mazingira, kufanya usafi na kuwapeleka shule watoto wao kuanza darasa la kwanza na kidato cha kwanza mwaka huu na kuonya watakaokaidi watakamatwa na kufikishwa

Diwani wa Kata ya Kwamkabara, Peter Mgavilwa aliishukuru NIDA kwa kuwapelekea wananchi vitambulisho.

Ofisa Msaidizi wa NIDA Wilaya ya Muheza, Prisca Mbaga aliwaahidi wananchi waliosajiliwa, vitambulisho vyao vitachapishwa na kuvipata muda mfupi ujao.

Ofisa Uhamiaji wa Wilaya ya Muheza, Amour Mohammed, alisema kitambulisho cha NIDA kina faida nyingi ikiwamo kupata pasi ya kusafiria, viza na utambulisho wa Mtanzania nchi za nje.



## HABARI KANDA YA ZIWA

# Ofisa elimu kortini kwa vifo vya watu watatu

**Na Vitus Audax,** KWIMBA

OFISA Elimu Taaluma wilayani hapo, Mkoa wa Mwanza, Samwel Kulinga (44), amefikishwa mahakamani kujibu mashtaka ya kuwagonga watu watatu na kuwasababishia vifo.

Mshtakiwa huyo alifikishwa jana katika Mahakama ya Wilaya Kwimba mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Dustan Ndeko.

Na kusomewa mashtaka manne naWakili wa Serikali, Frank Nchanila.

Wakili Nchanila alimsomea mashtaka mengine mshtakiwa huyo kuwa ni kuendesha gari lake binafsi aina ya Toyota Wish bila kuwa na leseni katika barabara ya umma, kuendesha kwa mwendo kasi, kuwagonga watu hao na kuwasababisha vifo.

Aliwataja waliokufa katika ajali hiyo iliyotokea eneo la Ilamba, Desemba 30 mwaka kuwa ni mwendesha baiskeli, Shauri Masasi (62), Robert Matata (35) na Sarah Faustine (43).

Kwa mujibu wa wakili huyo, mshtakiwa huyo anakabiliwa na mashtaka hayo kinyume na sheria za usalama barabarani.

Mshtakiwa huyo yuko nje kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya kuwa na mdhamini mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa kiongozi wa Serikali za Mitaa na mwingine mwenye mali isiyohamishika yenye thamani ya Shilingi milioni 5 na nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) cha mpigakura.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Februari 19, mwaka huu kwa mshtakiwa huyo kuanza kusomewa maelezo ya awali.



Ofisa Elimu Taaluma wa Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza, Samwel Kulinga akishuka kwenye ngazi za Mahakama ya wilaya hiyo jana baada ya kusomewa mashtaka manne, ikimemo kuendesha gari kwa mwendo kasi na kuwagonga watu watatu na kuwasababishia vifo. **PICHA: VITUS AUDAX**

## Wafunzwa ulinzi shirikishi

**Na Timothy Itembe,** RORYA

JESHI la Polisi Wilaya ya Kipolisi Shirati mkoani Mara limetoa mafunzo ya ulinzi shirikishi kwa wakazi wa Kata ya Nyahongo, Tarafa ya Nyancha, kwa lengo la kudhibiti uhalifu na kujichukulia sheria mkononi.

Mbali na kutoa mafunzo hayo, jeshi hilo na wakazi hao, wameingia makubaliano ya kufichua vitendo vya uhalifu na wahalifu bila kujichukulia sheria mkononi ili kulinda na kudumisha amani na utulivu katika wilaya yao.

Akizungumza wakati wa utoaji mafunzo hao katika vijiwe vya mitaa ya wilaya hiyo, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, David Chambala, aliwataka wakazi hao kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo, kuondoa hofu ya kuvuja siri dhidi ya wahalifu na uhalifu.

Chambala, alisema taarifa zitakazotolewa dhidi ya vitendo hivyo na wanaojihusisha navyo, zitatumika kuimarisha ulinzi katika jamii ya wakazi hao, kuyafikia maeneo yenye viashiria vya uhalifu na kudhibiti kwa wakati.

Aliwataka kuwa na amani wanapotekeleza jukumu la ulinzi shirikishi kwa kuwa jeshi hilo, litakuwa bega kwa bega kudhibiti uhalifu utakaoripotiwa na wananchi.

"Mnachotakiwa ni kushirikiana na wenyeviti wa vitongoji katika maeneo yenu kukemea uhalifu na wahalifu, katika kufanya hivyo naomba msitumie nguvu ya kujichukulia sheria mkononi," alisisitiza Chambala.

Alionya kuwa ni kinyume cha sheria kwa mtu yoyote kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa hakuna mtu anayeruhusiwa kumpiga wala kumwadhibu mtuhumiwa, bali ni kutoa taarifa ili akamatwe na kufikishwa mahakamani.

Baadhi ya wakazi hao walidai kuwa wanapowakamata watuhumiwa, wanatoa taarifa kwa jeshi hilo ili wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Thobias Obwasi, ambaye ni fundi viatu, alidai kinachowakwamisha kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu kwa jeshi hilo ni kukosa imani na kuvuja kwa siri zao.

Alisema kutokana na jeshi hilo kuwahakikishia ulinzi na usalama, wapo tayari kuwataja wahalifu ili kuhakikisha wanaishi kwa amani katika maeneo yao.

Aliliomba jeshi hilo kutoa taarifa ya watuhumiwa wanaokamatwa ili kuongeza imani kwao na kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwao hao huachiliwa na kurudi mitaani kuendeleza uhalifu na kuhatarisha usalama wao.

## TAKUKURU yaibua ubadhirifu miradi ya maendeleo

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani hapa inachunguza ubadhirifu wa zaidi ya Shilingi bilioni 1.5 katika ujenzi wa miradi minne ya maendeleo kutokana na kusuasua na kujengwa chini ya viwango.

Mianya hiyo ya ubadhirifu kwenye miradi hiyo kati ya 14 yenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 6.4 inayojengwa mkoani hapa imebainika kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka jana.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Geita, Azza Mtaita, aliitaja miradi hiyo yenye ubadhirifu kuwa ni ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Nyantorotoro uliogharimu zaidi ya Sh.milioni 584, Shule ya Msingi Nyantorotoro Sh.milioni 181na kituo cha mabasi Ikangala.

Alisema ujenzi wa majengo ya Shule ya Mseveni Chato unaogharimu zaidi ya Sh.bilioni 1.5 uko chini ya kiwango na hauendani na thamani ya kiasi hicho cha fedha zilizotumika.

Mtaita, alisema baada ya TAKUKURU kukamilisha uchunguzi huo, watuhumiwa watakamatwa na kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka ya uhujumu uchumi.

Amewaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa kufichua vitendo vya rushwa na kutoa taarifa za viashiria vya vitendo hivyo katika maeneo ya kutolea huduma zikiwamo hospitali, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Jeshi la Polisi na maeneo ya umma na binafsi.

Alisema kupitia Programu ya TAKUKURU Rafiki, wameibua kero 242 katika kata 19 mkoani hapa, kati ya hizo 55 zimepatiwa majibu na 187 kuwasilishwa idara husika kupatiwa ufumbuzi.

Kwa upande mwingine, Mtaita, aliwatahadharisha wananchi mkoani hapa kuepuka watiania walioanza kuwashawishi kwa kuwapa zawadi kabla ya majina yao kupitishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwania uongozi katika chaguzi zijazo nchini.

## Watanzania 'kuula' migodi nje ya nchi

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

UONGOZI wa Kampuni ya uchimbaji madini ya Barrick umeanza mchakato wa kupeleka Watanzania kushika nyadhifa za uongozi kwenye migodi yake iliyopo nje ya nchi.

Barrick inamilikiwa kwa ubia na serikali migodi ya North Mara uliopo mkoani Mara na Bulyanhulu Shinyanga.

Akizungumza kwenye mgodi wa Bulyanhulu wakati akiwasilisha ripoti ya utendaji yo robo mwaka, Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Dk. Mark Bristow alisema kuwa lengo ni kuwaongezea ujuzi na uzoefu raia hao wa Tanzania kwa kufanya kazi katika nyadhifa hizo nje ya nchi.

"Nimefurahishwa sana na mazingira ya uwekezaji chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, na hii imepelekea sasa kupeleka Watanzania kwenda kupata ujuzi zaidi katika uendeshaji wa migodi katika migodi yetu nje ya Tanzania," alisema Bristow.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwa na wataalamu wengi Watanzania kwenye sekta ya uchimbaji madini watakaosaidia kuiendeleza.

Barrick pia inamiliki migodi ya uchimbaji madini katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Ivory Coast, Chile, Marekani, Canada, Argentina na Jamhuri ya Dominica.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa hiyo, Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, alipongeza hatua hiyo ya kupeleka Watanzania kupata uzoefu kwenye migodi hiyo ya nje ya nchi.

Kiruswa, alisema serikali inajivunia uwekezaji wa ubia na Barrick na matunda yake yanaonekana wazi.

"Ni hatua nzuri sana kwa Watanzania, hii itasaidia sana kuwa na wataalamu wengi katika sekta ya madini, nawapongeza sana," alisema.

Wakati huo huo; Naibu Waziri huyo ameziagiza kampuni nyingine zenye ubia na Serikali kuweka utaratibu wa kutoa ripoti ya utendaji kazi kwa wananchi kupitia mikutano ya pamoja kama wanavyofanya Barrick.

"Makampuni mengine natoa maagizo waandae utaratibu kama huu wa kutoa ripoti zao kila baada ya robo mwaka, hii itasaidia kuona ni namna gani utendaji unafanyika na wananchi waone mafanikio yake," alisema Kiruswa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Barrick imetumia zaidi ya Shilingi bilioni 35 kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo nchini.

ama
ALHAMISI FEBRUARI 1, 2024
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

## Simulizi ya TB Manyara, ukweli wa magumu yanayowapiga wazee, watoto



## TB ilivyo 'pasua kichwa' Kigoma, wenyeji kipaumbele chao tiba asilia

Ukurasa 13

# Samia Outreach Service; mradi mpya unaoendeleza ubunifu wa Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI sasa serikali inatumikia awamu ya sita, mhimili wa chama kile kile tangu kupatikana uhuru, ilikoanza na vyama vingi, kisha sera ya chama kimoja ikadumu kwa miaka 28, kabla ya kurejea vyama vingi mpaka sasa, mhimili unaotawaliwa ni wa chama kilichoipatia nchi uhuru.

Kisera, ndani yake ni mwendelezo wa ilani na sera, viongozi wakipokezana kijiti cha uongozi, kila mmoja akiboresha alikoshia mtangulizi wake.

Kikubwa hapo, alishalitolea ufafanuzi kuhusu maboresho Mzee Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili kwamba 'kila zama na azma zake' na ndiyo kwenye mzizi wa kwanza, mageuzi na maboresho ya kiungozi yanayofanyika bila ya kupoteza falsafa walioanza nayo.

Tofauti kubwa inakuwa katika mahitaji ya wakati na hulka za kiuongozi, maana iko wazi watu wote hawafanani, ingawaje binadamu wote ni sawa.

Leo hii, kuna la kipekee kwake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita. Akiendeleza kijiti cha mwasisi Mwalimu Julius Nyerere, aliyesisitiza maboresho katika elimu, afya na uzalishaji hasa shambani, kuna staili anafanya katika sekta ya afya, hata kuwa kivutio cha umma na nchi jirani, bila kusahau itikadi ya jinsia.

Kwa sasa, ameamua kuwekeza kwa kina elimu katika kundi la matabibu afya ili kuwa na wataalamu wengi mabingwa wanatatua shida za kiafya za Watanzania, huku nao wakisambaza ujuzi huo kwa wataalamu wenzao wote wa afya nchini.




Watumishi wa Hospitali ya Rufani Kigoma, wakipokea msaada uliotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mwaka 2022. **PICHA: MTANDAO**

Hapo Dk. Samia anatumia mtaji wa Mpango wa Elimu ya Afya ya Msingi (MMAM), aliyoubuni Rais Jakaya Kikwete wa awamu ya nne, awamu ya sita 'ikidurufu' idadi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali kitaifa, ili zitapakae kila Mtanzania afikiwe kirahisi aliko.

Kwa mujibu wa MMAM iliyoanza kutekelezwa rasmi 2008, kila kijiji au kitongoji kinapaswa kuwa na zahanati, kata ina kituo cha afya, wilaya hospitali na mkoa kwenda juu ni hospitali za rufani.

Serikali inaboresha mfumo huo unaoangukia tafsiri ya Rais Nyerere 'kuboresha elimu na afya' mabingwa tiba kutoka hospitali za rufani na taifa kama vile Muhimbili, Dodoma, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete na na Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), huweka kambi katika hospitali za chini yao kueneza ujuzi.

Hiyo ni zao la elimu mabingwa hao wanapata, ikijumuisha ya teknolojia na vifaa vya kisasa, hali kadhalika stadi mpya zinazovumbuliwa kimataifa, hospitali za chini zao la MMAM, zikipatiwa vifaa na ujuzi wa ziada kuwahudumia wagonjwa wao.

Mathalani hadi sasa, huduma zitokanazo na vifaa vya CT scan zilizokuwa hadimu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu anasema ziko kote kitaifa, huku huduma nyingi zilizofuatwa nje ya nchi, sasa zinapatikana nchini, kuwapatia nafuu wagonjwa na serikali katika gharama.

Hilo linaendelea, huku Dk. Samia, akitamka kuendeleza falsafa yake ya kuongeza bajeti maradufu inayoboresha sekta ya afya. Ni dhana ya Rais Nyerere, katika azma za sasa, sekta afya na elimu kupitia afya ikipaa maradufu.

### USHUHUDA ULIKO

Hatima inayoshusha huduma za stadi za juu kuwafikia wahitaji, Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel, anaifafanua "Serikali ya Awamu ya Sita imetenga shilingi trilioni 6.7 za kuboresha huduma za afya."

Hapo anataja kusomesha wataalamu ndani na nje ya nchi, kuwezesha huduma za kibingwa kufika mbali waliko wahitaji.

Kauli yake anaitoa katika tukio la utekelezaji mwongozo huo katika Hospitali ya Wilaya ya Siha, Kilimanjaro, ambako huduma za kibingwa za uchunguzi matibabu ya moyo zilizotolewa na wataalamu wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na wenzao wa hospitali hiyo kwa siku tatu.

"Kama hawa watu waliogundulika kuwa na matatizo wasingeonwa katika kambi hii, si ajabu wasingeweza kuishi muda mrefu, lakini uwepo wa matibabu haya umewasaidia kugundulika kuwa na matatizo ambayo yanahitaji matibabu ya kibingwa na watapata matibabu mapema.

"Huduma za matibabu zinazopatikana katika upimaji huu zinatolewa bila malipo yoyote yale, kwani serikali imegharamia kila kitu na kutokana na uhitaji kuwa mkubwa JKCI wameongeza siku mbili..." akatamka Dk. Mollel, ambaye ni tabibu kitaaluma, pia mbunge wa Siha.

Kwa muda wa siku tatu hizo, wataalamu wakaona watu 307 kati yao 37 wamekutwa na matatizo yanayohitaji matibabu ya kibingwa, hivyo kupewa rufani ya kwenda kutibiwa katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Dk. Peter Kisenge na Mkurugenzi wa Tiba Shirikishi wa JKCI Dk. Delilah Kimambo, wakafafanua, taasisi hiyo imekuwa ikitoa huduma ya tiba mkoba ijulikanayo 'Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan Outreach Services' wakiwafuata wananchi mahali kuwatibu kibingwa.

Pia, tiba mkoba inatoa nafasi kwa wanaokutwa na matatizo ya moyo, wanatibiwa mapema wakipewa rufaa na kuwajengea uwezo wataalamu wa hospitali husika, ili baada ya kumalizika kwa kambi ya matibabu, nao waweze kuwatambua na kuwatibu wagonjwa wa moyo.

AFYA

# Simulizi ya TB Manyara na ukweli wa magumu yanayowapiga wazee, watoto

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

HADI sasa, watoto wachanga na wajawazito ni makundi yanayoangaliwa kwa karibu na jamii pamoja na serikali, ingawa ndio yanashambuliwa na maradhi kifua kikuu (TB). Shida ilipo inatajwa uelewa duni wa jamii.

Inaporejewa jamii, mkazi wa Mtaa wa Kitalu X, Musa Rehani, mzee mstaafu anasimulia zamani watu waliugua TB, ila walikuwa wachache, hata walipougua walikaa majumbani wakijitibu kwa dawa asili.

"Zamani mgonjwa akikohoa makohozi, ilikuwa inachukua siku tatu mpaka wiki moja kupata majibu ya vipimo alivyofanyiwa, ila siku hizi vipimo vinachukuliwa na majibu unapata hapo hapo,"anaeleza Rehani

Anasema watu sasa wana uelewa mkubwa, hata wakiona tatizo la namna hiyo, wanalifanyia kazi haraka na kwa watoto, anasema kinga zao sasa ziko chini kuliko wa zamani walioenda shule bila sweta na miili yao ilikuwa imara, kulinganisha na watoto wa sasa.

Mstaafu huyo anasema, matibabu ya zamani yalikuwa bure kwa wote, bima za afya hazikuwapo, hivyo matibabu yalikuwa rahisi.

Mkazi wa Kijiji cha Magugu, Husna Ramadhan, anasema TB wanaugua wazee pekee, wanaokohoa kila mara, ila hajui matibabu yakoje.

Husna anasema, TB inawapata zaidi watoto na hajawahi kupata elimu hiyo kutoka kwa wataalamu wa afya.

Mkazi wa Mtaa wa Miomboni, Paschal Masaay, anaushuhuda kifua kikuu kinavyoambukiza kwa njia ya hewa, baada ya mgonjwa kukohoa, vilevile inawapata wazee mara nyingi, lakini anadai kutofahamu maambukizi kwa watoto chini ya miaka mitano.

Mkazi wa Kijiji cha Daghailoy, Kudra Moses, anasema anasikia TB kwenye vyombo vya habari inavyoambukizwa kwa njia ya hewa, ila hajui kama inavyowapata watoto.

Anatumia fursa hiyo kuiomba serikali itoa elimu kuanzia ngazi ya kitongoji mpaka taifa, ili wananchi waielewe na namna ya kujikinga nao.




Wananchi wa wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wakipatiwa elimu ya ugonjwa wa kifua kikuu na wataalamu wa Afya. **PICHA: JALIWASON JASSON**

**WATAALAMU WANENA**

Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma Mkoa wa Manyara Dk. Mandala Adamm, anasema Tanzania imo katika nchi 30 zenye wagonjwa hao na mkoa wa Manyara mwaka 2020, ulikuwa wa tano kuwa na wagonjwa wengi kitaifa.

Mwaka jana anasema, ukawa mkoa wa 10 baada ya kupunguza idadi ya wagonjwa na mwaka jana mkoa ukajiwekea lengo la kugundua wagonjwa wa TB 3,688. Mpaka Disemba mwaka 2023 ilishabaini wagonjwa 3,992.

Hao ni watoto wa miaka 14, kushuka hadi mitano waliokuwa 1,490 na umri miaka mitano na kushuka waligundulika 332.

Anaeleza, wagonjwa wanawake bila kutenganisha wajawazito na wasio wajawazito waligundulika 2,003 kwa kipindi hicho.

Mtaalamu huyo anasema, watoto wadogo hupata maambukizi kutoka kwa watu wazima wanapozaliwa, sabau kinga zao zinakuwa haijakomaa. Anataja njia zinazotumika kuwakinga watoto na TB ni chanjo anayopewa, baada ya kuzaliwa.

Daktari huyo anasema, dalili kwa watoto ni kushindwa kuongezeka uzito au kupungua uzito, akisema TB na lishe duni huendana.

"Mtoto akija ana lishe duni, lazima afanyiwe uchunguzi wa TB, ili tuone tatizo lake kama kweli ana TB,"anasema Dk. Adam

Pia, anataja dalili nyingine, ni mgonjwa kuwa na homa za kila mara, usiku analia na kukosa hamu ya chakula, vilevile uvimbe shingoni.

Mratibu Dk. Adam, anasema huwa wanawachunguza kupima makohozi au hajo kubwa kubaini 'vijidudu' husika.

Anasema TB inaweza kumpata kila mtu, mtoto au mtu mzima, ila watoto na wazee wako kwenye hatari, maana kinga zao ziko chini.

Wengine walio hatarini anawataja ni wagonjwa wa kisukari, virusi vya Ukimwi na wanaoishi kwenye msongamano.

Dk. Adam anasema zamani matibabu yalichukua miaka miwili, sasa ni miezi sita tu,wakitumia dawa mseto, miezi miwili ya kwanza mseto wa dawa nne; miezi minne inayofuata dawa mbili, jumla siku 168 sawa na miezi sita.

Anafafanua, tiba ya mtoto iko tofauti, dawa zina ladha ya machungwa inayomfanya mtoto aipende.

**KWA MTOTO TUMBONI**

Mtaalamu huyo wa afya, anasema inawezekana pale vijidudu vinashambulia mji wa mimba na kwenda kwa mtoto.

Anasema, mjamzito anapogundulika mapema akaanza kutumia dawa, atakingwa na mtoto kutokupata TB.

Mratibu wa TB, Dk. Adam anasema wajawazito wako hatarini kwa maradhi hayo, akiwashauri wafanyiwe uchunguzi wa matibabu yanatolewa bure.

Pia, kuna baadhi ya wadau wanaosaidia kutoa elimu na tiba, wakijumuisha vyombo vya habari, vituo vya afya, watoa huduma ngazi ya jamii mradi kama wa Usaid Afya Yangu', kupitia Shirika la Elizabeth Glaser Pediatric Aids Foundation (EGPAF) wanawasaidia kutekeleza.

**MAGUMU YANAYOWAKABILI**

Anataja imani potofu, wakiwapo wanaoamini TB ugonjwa wa kulogwa, wanatumia muda mrefu kutumia dawa za asili na ili kudhibiti hilo, wanatajwa kuwawezesha watu wa tiba mbadala kusaidia kugundua wenye TB.

Kikwazo kingine kinatajwa, ni uelewa mdogo kwa kuwapo wanaoamini kifua kikuu ni maradhi ya watu maskini na Dk. Adam anasema, hata mgonjwa anapoenda hospitalini kwa maradhi tofauti.

Hapo mgonjwa huulizwa yanayohusiana na kifua kikuu, lengo ni kujitahidi kufikia maradhi hayo ndani ya jamii.

Jitihada nyinginezo anataja ni kuwatumia watoa huduma ngazi ya jamii wanatembelea makazi, pia hadi magerezani, kwenye machimbo na kambi za wavuvi, wakitoa elimu.

Anasema utafiti unabainisha vifo vya watoto na wajawazito vinasababishwa na TB, pia virusi vya Ukimwi jumla yake asilimia 10.

"Mjamzito tukimbaini akiwa katika kipindi cha kwanza mpaka kipindi cha tatu tunamuanzishia dawa za TB," anaeleza Dk. Adam.

Anafafanua namna ya tiba, tofauti ni mgonjwa wa kipindi cha tatu atakapojifungua, hatapewa 'chanjo ya TB' bali 'tiba kinga ya TB.'

Pia, Dk Adam anaeleza mgonjwa akikamilisha 'tiba kinga' ya miezi sita, anapatiwa chanjo ambayo hakupewa wakati wa kuzaliwa mtoto.

Mtaalamu huyo anasema, kwa sasa tiba kinga inatolewa kwa muda wa miezi sita, japo ndani ya mwaka huo, nchini kutaanzishwa tiba kinga ya TB ya miezi mitatu.

Pia, anaeleza zamani wagonjwa wote ilikuwa wadungwe sindano 60 kwa miezi sita, ila sasa hivi inatolewa dawa na matibabu ya miezi sita na siyo miaka miwili.

Daktari huyo pia anazungumzia, namna tofauti iliyopo kwa tiba ya kawaida na sugu, ambayo ni vimelea vinakuwa vigumu kumalizika.

Ugumu wa kupona TB, pia inatajwa ni pale mgonjwa anaacha tiba, kabla hajatimiza miezi sita, daktari huyi akifafanua: "Matibabu ya TB sugu huchukua miezi tisa mpaka miezi 24 ila dalili ni zile zile za TB."

Kuhusu matibabu kwa hospitali binafsi, anasema kote yanatolewa bila ya malipo, serikali inagharamia, japo anasema wagonjwa wengi wa TB hueenda kwenye vituo vya serikali.

Mratibu huyo anasema, wagonjwa wengi kwa mkoa Manyara, wanapatikana Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto na Simanjiro, ikifuatiwa na wilaya ya Mbulu.

Halmashauri nyinginezo ni; Babati, Hanang' na Halmashauri ya Mji wa Babati, akitoa takwimu za mfano, Kiteto kunafanyika jitihada za kuwapata wagonjwa, Dk.Ada, akitaja mwaka jana, Kiteto peke yake imekuwa na wagonjwa 1000 wa TB.

Anafafanua kifua kikuu kuwa ugonjwa wa kuambukiza hatari, maana wengi katika jamii wanatumia usafiri wa umma.

Dk. Adam anaiomba jamii iendelee kutoa ushirikiano kwa watoa huduma ngazi ya jamii na jamii iendelee kupokea tiba kinga kwa makundi hatarishi mfano wenye VVU, watoto chini ya miaka mitano wanaoishi na wagonjwa wa TB.

**NENO LA WADAU**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Misheni Dareda inayomilikiwa na Kanisa Katoliki, Jimbo la Mbulu, Dk. Joseph Lorri, anakiri kupokea wagonjwa wa TB na kuwahudumia bure.

Anasema kundi kubwa ni la wazee, pia wapo watoto wa umri chini ya miaka mitano na wajawazito wanapokelewa wakiwa na TB.

Dk. Lorri anasema, watoto wagonjwa huwa mara nyingi wanakuwa wameambukizwa na wazazi, pia mara nyingi ni watoto wenye lishe duni.

"Lishe duni ni chanzo cha TB hivyo mzazi akiona mtoto anapungua uzito achukue hatua na watoto. Wakati mwingine, tunawagundua wanapoletwa kliniki," anasema Dk. Lorri, akigusia ugumu wa kuchukua makohozi ya vipimo kwa watoto hao.

Mtaalamu huyo wa afya, anasema mbadala wanatumia ni kupata majibu kwa vipimo vya kinyesi cha mtoto.

Ripoti ya Shirika la Elizabeth Glaser Pediatric Aids Foundation (EGPAF) ya mwaka jana, inasema watu milioni 10 wanaumwa TB kila mwaka duniani na kati yao, watu 4000 wanakufa na TB kila siku.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2021 ilibaini watoto Mil. 1.2 waliendelea kuwa na TB na asilimia 14 yao walikufa.

WHO inasema, TB inasababisha vifo vya watoto na mojawapo ya vyanzo 10 vya vifo vya watoto duniani.

- **Kwa mawasiliano na mwandishi wa makala: +255 787598182.**

AFYA

# TB ilivyo 'pasua kichwa' Kigoma, wenyeji kipaumbele chao tiba asilia

**Na Adela Madyane -Kigoma**

HADI sasa Mkoa wa Kigoma unatajwa kuwa na wagonjwa wengi wa kifua kikuu (TB), wakiongezeka kila mwaka, sababu kuu ni kukosekana taarifa sahihi.

Ni maradhi yanayoambukiza zaidi mapafu, pia sehemu nyinginezo za mwili kama vile mifupa, hata uti wa mgongo.

TB huwa juu zaidi, pale kinga ya mwili zinashuka kutokana na sababu kama za uzee, lishe duni na magonjwa kama kansa, kisukari, Ukimwi. Ni bahati mbaya, mkoani Kigoma imani duni ipo juu zaidi.

Ni ugonjwa unaoambukiza kutoka mtu mmoja, hadi mwingine kupitia hewa, mgonjwa anapokohoa au mate yake yakiwa hewani, bakteria wanaojulikana 'Mycobacteria' wanasambaa.

Dalili zake zinatajwa; kukohoa mfululizo wiki mbili hadi tatu na wapo wanaokohoa damu, wanapoteza hamu ya kula, uzito unapungua ndani ya miezi mitatu, pia wakitokwa jasho jingi usiku, uchovu, maumivu makali ya kichwa na kifua, wanapumua kwa shida, homa za kila mara.



Tukio la kukabidhiwa vifaa vya maabara (Hadubini), vilivyotolewa na Shirika la Tanzania Health Promotion Support (THPS) vyenye thamani ya Sh. milioni 35 kwa ajili ya kuimarisha tiba ya kifua kikuu, mkoani Kigoma. **PICHA: MAKTABA**

### HOJA YA MTAALAMU

Mratibu wa Huduma za Kifua Kikuu na Ukoma Mkoa wa Kigoma, Dk. Enock Mwantala, anafafanua sababu za kuongezeka wagonjwa ni wananchi kukosa elimu sahihi inayohusu kifua kikuu.

Anatoa mfano kati ya Oktoba 2022 na Juni 2023, wagonjwa watano walikutwa kwa mganga wa kienyeji, wakati wa ziara za wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

Anasema mwaka 2020, wagonjwa 78 wa kifua kikuu walifariki Kigoma na mwaka unaofuata, vifo 66. Dk. Mwantala anaendelea: "Mwaka 2021 tulikuwa na mgonjwa mmoja wa kifua kikuu sugu na 2022 tulikuwa na wagonjwa wanne.

"Kuanzia Januari hadi Julai 2023, kulikuwa na wagonjwa wa kifua kikuu sugu 14, jumla yao 1,106. Unaweza kuona namna gani kuna ongezeko la wagonjwa siku hadi siku."

Anataja takwimu za wagonjwa mkoani humo: Mwaka 2021 walikuwa 1,492; 2022 wakafikia 1,604; na hadi Julai mwaka jana walikuwa 1,106.

Dk. Mwantala anafafanua wagonjwa wengi wa TB, huenda kwenye tiba asili, bila kujua suluhisho liko hospitalini, ambako baadhi hufikishwa katika hali mbaya, hata wanapopoteza maisha au kupata usugu, dawa zinashindwa kufanya kazi.

"Tunaomba jamii ifahamu kuwa ugonjwa wa kifua kikuu unatibika na kupona kabisa na matibabu yake pamoja na uchunguzi ni bure, ambayo yanatolewa kwenye kituo chochote kile kinachotoa huduma za afya," anasema Mratibu Dk. Mwantala.

### MSAADA UNAOWAFIKIA

Dk. Mwantala anasema, Kigoma inasaidiwa na mradi wa Shirika la Marekani - USAID, Afya Shirikishi na Shirika la Amref Health Africa, Tanzania.

Mtaalamu, Elly Josephat anasema ni mradi unaotekelezwa na shirika hilo kwa kushirikiana na serikali, lengo kukabili kifua kikuu, pia uzazi wa mpango kwa jamii.

Anasema kwenye kifua kikuu, mradi umejikita kutambua wagonjwa na kuwaanzishia matibabu, hasa kwa walio hatarinii.

Josephat anaeleza wanavyowafuata walioacha matibabu kujua sababu zao, kisha wanawarudisha kuendelea na dawa.

Kufanikisha hilo, anasema wanawatumia wahudumu afya 98 ngazi ya jamii waliowachagua katika halmashauri zote za mkoa, kisha wakawapatia mafunzo.

Josephat anasema, hilo wanashirkiana na waganga wa jadi, kutokana na jamii zinazowazunguka kuamini zaidi tabibu za jadi, kuliko hospitalini, hivyo waganga asilia wanakuwa madaraja kuwaunganisha kufanikisha kuchunguza afya za wanajamii.

"Tunafanya kazi pia na wauza maduka ya dawa ambao wameunganishwa na wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

"Pindi wanapopata mteja mwenye kikohozi au dalili za kifua kikuu wanamuunganisha na mhudumu wa afya kwa ajili ya uchunguzi zaidi na kufatiliwa," anasema Josephat, anayekiri kuwapo unyanyapaa unaoendana na imani potofu.

### IMANI POTOFU

Kuhusu ushirikina, Nipashe ikakutana na ndugu wa marehemu (jina tunalo) aliyefariki, akiwa na madai amelogwa.

Marehemu huyo mkazi wa kijiji cha Mahembe, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, alifariki kwa kukosa huduma stahiki za TB, akijielekeza kwa waganga wa kienyeji.

Inaelezwa, alianza kuugua akikosa nguvu mwilini akashindwa kula na akikohoa sana na walipoenda maabara, vipimo vikaonyesha 'ana kikohozi' na akapatiwa dawa za maumivu na kikohozi, kutuliza maumivu yake.

Hata hivyo, inaelezwa aliendelea kuwa na hali mbaya na hali mbaya, ndipo akaamua kwenda kwa waganga wa kienyeji akiamini amelogwa.

Safari hiyo akaambatana na rafiki yake, Siajalii Athuman, aliyemuuguza kwa mganga mwezi mmoja pasipo nafuu, afya ikiendelea kuzorota hadi baadhi ya ndugu walipomchukua, kuhamia Hospitali ya Wilaya ya Baptist, Manispaa ya Kigoma Ujiji, ambako umauti ulimfika akihudumiwa.

Siajalii anasema, rafikiye alipendelea kuvuta sigara za kienyeji na kutumia ugoro, visababishi vya TB, huku mganga wa kienyeji akiwaambia amelogwa katika 'mfumo wa hewani' na ana uwezo wa kumtibu, kurejesha hali ya kawaida.

Ntahonkiliye Kayanda, jirani wa marehemu anasema alimshawishi kwenda hospitali kubwa kwa vipimo zaidi, lakini alikataa akidai yeye maskini hatomudu gharama, akijielekeza kwa tiba asilia na binafsi aliifahamu miti tiba, wangesaidiana kufanikisha matibabu.

Kaka wa marehemu, Kiheke Masoud, anaonyesha masikitisho, dada yake kuegemea ushirikina, badala ya hospitalini, Masoud akieleza:

"Nilimkuta dada akiwa katika hali mbaya, alikuwa anakohoa sana, mwili wake ulidhoofika sana. Nilikasirika nikaamua kumtoa kwa mganga na kumpeleka hospitali, kutokana na afya yake kuwa mbaya hakuchuka muda mrefu alifariki dunia."

### MGONJWA AELEZA UZOEFU

Mgonjwa wa kifua kikuu, Issa Kiza, anasema alianza kuumwa Novemba 2022, akaanza matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Kigoma Januari mwaka huu, afya yake ikiwa katika hali isiyoridhisha.

Kiza anasema, alianza kutumia dawa za kifua kikuu na kwa sasa anaendelea vizuri, ikilinganishwa na alipoanza tiba, amedhoofika.

Akizungumzia unyanyapaa, anasema bado jamii inashindwa kutofautisha kifua kikuu na magonjwa mengine, hata kuwafanya wadhihakiwe.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kifua kikuu kinaambukiza watu milioni 10 na kuua watu milioni 1.5 kila mwaka, hivyo kuwa muuaji wa pili wa magonjwa ya kuambukiza baada ya Covid-19.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu Julai 4, 2023 alifungua Mkutano wa Makatibu Wakuu na Mameneja Mpango wa Programu za Kifua Kikuu wa nchi 15 Afrika, uliofanyika siku tatu jijini Arusha, lengo kujadili ubunifu na mikakati mpya Afrika inaweza kutumia kutokomeza TB, ifikapo mwaka 2030.

Akauambia mkutano, watu 70 hufariki kila siku nchini kutokana na ugonjwa huo jumla yao , 25,800 wakifikia hilo kila mwaka, akiwa na ufafanuzi: "Kwa kushirikiana na Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu, Ukimwi na Malaria tumeamua kukutana na Makatibu Wakuu wa Wizara za Afya, ili tujadili namna ya kuutokomeza ugonjwa huo ifikapo 2030," anasema.

Wizara ya Afya ya mwaka 2023/24 imetenga kiasi cha Sh trilioini 1.2, kutekeleza Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu, ambayo inatarajia kuibuaji wagonjwa wa TB kwenye jamii na tiba kinga dhidi ya maradhi hayo, wakiwamo watoto wenye umri chini ya miaka mitano.



Dk. Elly Josephat, Mratibu wa Mkoa wa Kigoma, wa Mradi wa USAID Afya Shirikishi, akitoa ufafanuzi kuhusu maradhi ya kifua kikuu akiwa ofisini kwake. **PICHA: ADELA MADYANE**

AFYA

# Kijue kituo cha afya kinachong'ara kwa huduma, kliniki yake 'ikifurika'

- Mwalimu asiyekosa kumsindikiza mkewe
- Wodini kuna 'mwenyekiti wa hospitali'

**Na Christina Mwakangale, aliyekuwa Mwanza**

KITUO cha Afya Bulale, kipo wilaya ya Nyamagana, mkoani Mwanza. Hakijawahi kuwa na kifo kutokana na mama kujifungua tangu kianzishwe mwaka 2018. Motisha ipo kwa watu wanaotoa ushawishi kwa mjamzito, kujifungulia kituoni hapo.

Kuhudhuria kliniki ya Baba, Mama na Mtoto (RCH), kwa wakati ni miongoni mwa silaha kubwa zinazotajwa na wataalamu wa afya, kwamba husaidia kuondoa dalili za hatari kwa mjamzito.

Mahudhurio ya RCH katika kituo hicho kwa kipindi cha mwezi mmoja katika kliniki hiyo, yamekua kutoka mahudhurio 10 na kufikia 300 hadi 400.

Mwalimu Kasase Kulusanga anahudhuria kliniki pamoja na mkewe. Ngoro Deus, aliyepitia changamoto kadhaa akibainika na dalili za hatari, presha ikishuka na kulazwa kwa miezi minne, sasa anafurahia mtoto.

"Kwa taarifa ambayo tunayo hadi sasa hatujawahi kuwa na kifo cha mama hapa kituoni. Wakati tunaanza ilikuwa ni Kiniki ya Mama na Mtoto sasa tumeboresha ni Kliniki ya Baba, Mama na Mtoto," Mganga Mfawidhi Kituo cha Afya Bulale, Dk Wambura Wanchoke.

Mwalimu Kasase Kulusanga (pichani), ni mkazi wa Bulale, Kata ya Buhongwa, wilaya ya Nyamgana, mkoani Mwanza. Amepanga foleni katika benchi kwenye Kliniki ya Baba, Mama na Mtoto, siku ya Jumatano wiki iliyopita. Anahudhuria kliniki, sambamba na mkewe.

Mahudhurio ya kliniki pamoja na mwenzi wake ni jambo la kawaida kwake. Anapewa kipaumbele na kupatiwa huduma na watoa huduma, akiwa na mkewe. Huo ni utaratibu wake wa kuambatana na mkewe kliniki tangu akiwa na mtoto mmoja sasa anao watatu.

Mwalimu huyo anayefundisha sekondari ya Nyalubogoya, iliyopo kata hiyo, baba wa watoto watatu, akiwa na mkewe katika kituo cha afya Bulale mkoani hapa, anasema tangu aanze kuhudhuria kwa ujauzito wa kwanza, hujiunga naye.

"Kila anapoanza kliniki mke wangu, nakuja naye kliniki, lengo ni kumtia moyo mama, kupokea ushauri kwa pamoja. Mimi ni mwalimu tena wa sayansi haya yote nayafahamu," anasema Kulusanga.

Anasema jamii ibadili dhana na kuhudhuria kliniki ya baba, mama na mtoto, kufahamu hali ya afya zao na kupata uelewa wa malezi kipindi cha ujauzito hadi kwa mtoto aliyezaliwa.




Mwalimu Kasase Kulusanga; daima hakosi kliniki na mweza wake.

"Kwanza kinachonishaiwshi na kunivutia kuhudhuria kliniki, ni kipaumbele tunachopewa wanaume ambao tumeongozana na wenza wetu. Utakuwa wa kwanza kupewa huduma. Hukai katika foleni hata kama umewakuta wengine.

"Pia namna huduma zinavyotolewa kituo hiki, kilianza ngazi ya zahanati hadi sasa ni kituo cha afya ninaona ufanisi wa huduma. Wanaume waache woga wa kuja kliniki na dhana iliyopo kwa baadhi yao, ni woga wa kipimo kikubwa," anasema mwalimu huyo.

Mwalimu Kulusanga ni miongoni mwa wenza 29 kati ya 221 waliohudhuria kliniki ya RCH Desemba mwaka jana, kituo cha afya Bulale.

**'MWENYEKITI' WA HOSPITALI**

Ngoro Deus, ni mkazi wa Kitongoji cha Mwahuli, wilaya hiyo, anapewa jina la utani na wahudumu wa kituo hicho kwamba, sasa aitwe 'Mwenyekiti wa Hospitali', akiwa mgonjwa pekee kukaa zaidi ya miezi minne mfululizo, kwa kulazwa hospitalini.

Anatoka wodini kwa mwendo wa taratibu. Ana saa chache tangu ajifungue mtoto wa kike. Katika mahojiano na waandishi, anasema amefanikiwa kujifungua mtoto huyo kwa njia ya kawaida, licha ya kupitia changamoto kadhaa, ikiwamo presha kushuka.

"Miaka mitatu imepita kabla ya mtoto huyu, nimejifungua kwa upasuaji, ila nilipofika hapa nikawaambia watoa huduma nitajifungua kawaida, na kweli wamenisaidia kujifungua kawaida,"anasema.

"Kabla huduma hazijaboreshwa tulikuwa tunasafiri umbali kidogo hadi hospitali ya wilaya ya Magu au ya Rufani Bugando ama Sekou Toure, sasa kituo hiki kimesaidia, nimelazwa hapa tangu Septemba mwaka jana," anasema Ngoro, akitabasamu.

**MABORESHO HUDUMA**

Maboresho ya huduma za afya kutoka zahanati Bulale iliyojengwa mwaka 2018 hadi kuwa kituo cha afya Bulale hivi sasa, imekuza kiwango cha utoaji huduma pamoja na kupunguza rufani katika hospitali za rufani.

Dk. Wambura Wanchoke, anasema jengo moja lilijengwa mwaka 2018 lilikuwa ni zahanati na kutoa huduma chache. Sasa huduma zimekua na hadhi kwa ngazi ya kituo cha afya.

Anasema mwaka 2023 baada ya kuongezwa watumishi, ujenzi wa majengo kama vile maabara, jengo la mionzi (radiolojia), jengo la kujifungulia pamoja na chumba cha upasuaji (theatre), sasa hadhi yake ni kituo cha afya.



Mgonjwa aliyedumu wodini mjamzito miezi minne katika Kituo cha Afya Bulale, Nyagamana, hata akabatizwa 'Mwenyekiti wa Hospitali.' **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**

"Kituo kimekuwa kikipokea fedha pamoja na mifuko mbalimbali mmojawapo ni wa Health Basket Fund (HBF)-Mfuko wa Afya wa pamoja nchini, kwa miaka miwili 2021 hadi 2023 tumepokea fedha takribani Sh. mil 11.

"Mwaka 2021/2022 tumepokea kama Sh. mil 4.8 na 2022/23 tulipokea kama Sh. mil 6.2 kwa ajili ya kusaidia utendaji kazi na mpango kazi uliokuwa nao. Asilimia 35 ya fedha huenda katika kununua dawa na vifaatiba, asilimia 15 motisha," anasema Dk. Wambura.

Kuhusu idadi ya watumishi wakati ikiwa zahanati Dk. Wambura anasema awali kulikuwa na wahudumu watatu pekee na ikafikia 10 baadae, lakini sasa imepanda hadhi ya kituo cha afya watumishi ni 36.

"Fedha nyingine hutumika kwa ajili ya kutoa huduma kwa watoto kwa huduma ya 'outreach' (kuwafikia pale walipo). Kadhalika kutoa huduma ya chanjo ya HPV (chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi). Fedha zingine tunawapa watu motisha kwa kuwaleta akinamama wajifungulie kituoni."

Kuhusu kumbukumbu za takwimu za wagonjwa wanaohudumia kituoni hapo, Dk. Wambura anataja namna zinavyoongezeka ikifika wagonjwa wa nje (OPD), wakiwa 200 hadi 300 kutoka 30 hadi 50 kwa mwezi hapo awali.

**MAJENGO MAPYA**

Kwa upande wa majengo, Dk. Wambura anasema yameongezeka ikiwamo la radiolojia, mama na mtoto, upasuaji, maabara na jengo maalumu la kufulia.

"Majengo haya yamesaidia kuchunguza wagonjwa wenyewe katika idara ya radilojia, yaani x-ray pamoja na ultra sound. Pia jengo la mama na mtoto, hasa wanaojifungua tunawafanyia upasuaji hapa hapa, tofauti na awali, ilipokuwa ni zahanati," anasema Dk. Wambura.

Anasema akinamama wanaojifungua katika kituo hicho imefikia 80 hadi 90 kwa mwezi kutoka 20 hadi 25 huku wanaojifungua kwa upasuaji tangu Julai mwaka jana, huduma ya upasuaji ilipoanzishwa ni 39 na hakuna kifo.

"Hatuna rekodi ya kifo cha mtoto, hii imetusaidia kuokoa maisha ya mtoto pamoja na mama. Serikali iendelee kuboresha huduma, ikiwamo maji," anasema Dk. Wambura.



HABARI DODOMA

# Serikali yatoa mabilioni huduma kupandikiza wenye Selimundu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 3.6 kwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH) kwa ajili ya kuanzishwa huduma ya upandikizaji uroto kwa wagonjwa wenye matatizo ya Selimundu.

Kutokana na uwekezaji huo, wagonjwa watatu wamepandikizwa figo na wanaendelea vizuri kiafya.

Akizungumza jana jijini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema upandikizaji huo kwa wagonjwa hao umefanikiwa kwa asilimia 100 na kwa sasa ni wazima.

"Kwa kweli historia imeandikwa kwa mara ya kwanza Hospitali ya Benjamini Mkapa imefanikiwa kupandikiza uroto kwa watoto watatu waliokuwa wakisumbuliwa na ugonjwa wa Selimundu," alisema

Dk. Chandika, alisema watoto waliopandikizwa uroto wamerudi shuleni kuendelea na masomo yao wakiwa na afya njema.

"Nawashukuru wazazi kwa kutuamini kuleta watoto wao hapa Benjamini kwa mara ya kwanza," alisema.

Dk. Chandika, alisema Tanzania ni nchi ya nne duniani kwa kuwa na watoto wenye Selimundu na kwa Afrika ya tatu. Alisema watoto 11,000 hugundulika kuwa na ugonjwa huo kila mwaka.

"Ugonjwa huu ni hatari sana , zaidi ya asilimia 50 wanaougua hawavuki miaka mitano hufariki, hata hao wanaovuka umri huo hawazidi miaka 45 hufariki ", alisema.

Mkurugenzi huyo, alisema serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa ajili ya matibabu ya ugonjwa huo kwani watoto chini ya miaka mitano wanatibiwa bure.

Alisema mpaka sasa watoto saba wamepatiwa huduma hiyo katika hospitali hiyo na hali zao zinaendelea vizuri.

Alisema baada ya kuona huduma hii muhimu inahitajika katika hospitalini hapo, Rais Samia Suluhu Hassan ameongeza tena Sh. billioni 1 kwa ajili ya kuboresha huduma hiyo.

Dk. Shakir Jumanne ambaye anahusika na masuala ya damu na wagonjwa wa Selimundu, alisema hospitali hiyo inajitahidi kusambaza dawa za kupunguza makali ya ugonjwa huo katika vituo vya afya .

Alisema watoto wanachaguliwa kupatiwa huduma hiyo kulingana na vigezo mbalimbali ikiwemo afya, kupatikana ndugu wa kuchangia damu.

Dk. Shakiri alisema serikali imepanga kuanza na watoto 20 ambao watapatiwa huduma hiyo hospitalini hapo kwa kushirikiana na madaktari kutoka nchini Italia

Elisha Osena, mmoja wa watoto waliopatiwa huduma hiyo hospitalini hapo, alimshukuru Rais Samia kwa kuanzishwaa huduma hiyo hospitalini hapo na kusema kuwa kwa sasa yeye ni mzima na anaenda shule kama kawaida.

"Nashukuru sana Rais Samia na Hospitali ya Benjamini Mkapa kwa matibabu waliyotupatia kwani nilikuwa nikipata maumivu makali ya mara kwa mara hata mahudhurio yangu shuleni yalikuwa mabaya, lakini kwa sasa mimi ni mzima," alisema Elisha




Mkurugenzi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Benson Ndiege (kulia), akibadilishana nyaraka na Ofisa Mkuu wa Tigopesa, Angelica Pesha jijini Dodoma jana, baada ya kutiliana saini mkataba wa makubaliano ya kulipa wakulima fedha zao za mazao kupitia miamala ya simu. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Wakulima wazidi kupata ahueni

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Chama cha Ushirika wa Wakulima nchini wameingia mkataba wa makubaliano (MOU) wa kimkakati na Kampuni ya Simu ya Tigo kwa ajili kurahisisha na kuimarisha miamala ya kifedha kwa wakulima wanaopokea malipo ya mazao kupitia jukwaa la miamala ya simu.

Makubaliano hayo ni mwendelezo wa ushirikiano kati ya Tigo Pesa, TCDC na chama hicho kwa dhamira ya kuimarisha jumuiya ya kilimo nchini.

Akizungumza kwenye hafla ya kusaini makubaliano hayo, Mrajisi wa Chama cha Ushirika nchini na Mkurugenzi Mtendaji wa TCDC, Dk. Benson Ndiege, alisema kufuatia kumalizika kwa mkataba wa miaka miwili mwaka jana, makubaliano mapya yanaashiria juhudi za kuimarisha ujumuishaji wa kifedha na kuwawezesha wakulima.

" Serikali kupitia TCDC inasubiri kwa hamu utekelezwaji wa MOU hii muhimu ili kuleta mapinduzi ya miamala ya fedha ndani ya sekta ya kilimo kupitia ushirika kuwawezesha wakulima na kukuza uchumi," alisema Ndiege.

Alisema ripoti ya hivi karibuni inaonyesha kiasi cha fedha kilicholipwa kwa miamala ya Tigopesa zao la cocoa  Shilingi milioni 800, Karafuu bilioni 11, Korosho bilioni 5, Mtama bilioni mbili na Choroko bilioni 20.

"Hapa inaonyesha makadirio ya fedha za wakulima zitakazokatwa kupitia miamala ya Tigopesa yanafikia Shilingi bilioni 20, hii inaonyesha namna gani ushirikiano huu utakavyokuwa na tija kukuza uchumi wa nchi yetu," alisema Ndiege.

Ofisa Mkuu wa Tigopesa, Angelica Pesha, alisema ushirikiano walioingia kwa mara nyingine unasisitiza dhamira ya kampuni hiyo  kuwezesha  miamala ya kifedha iliyo salama na ufanisi kwa sekta ya kilimo nchini.

"Chini ya masharti ya mkataba mpya, Tigo Pesa itaendeleza huduma zake za kutegemewa za fedha kwa njia ya simu kwa malipo ya mazao kwa wakulima wanaohusishwa na TCDC na Chama cha Ushirika cha Wakulima," alisema Angelica.

Alisema kampuni hiyo itaendelea kukuza ushirikishwaji wa kifedha, kusaidia uchumi wa ndani na kuchangia ukuaji wa sekta ya kilimo nchini.

Alisema ushirikiano huo mpya  unatumika kama ushuhuda na maono ya pamoja ya Tigo, TCDC, na chama hicho kuleta matokeo chanya kwa wakulima nchini.

# 'TEHAMA kuimarishwa taasisi za haki nchini'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria Dk. Pindi Chana amesema Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika taasisi za haki jinai nchini ili kuondoa malalamiko ya ucheleweshaji haki na rushwa .

Dk. Chana, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati wa hafla ya utoaji wa vifaa vya TEHAMA kwa taasisi za haki jinai nchini iliyofanyika mji wa kiserikali Mtumba.

Alisema serikali imepanga kufanya uwekezaji mkubwa katika taasisi za haki jinai nchini ili kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa na wananchi.

"Mifumo hii itasaidia sana kuondoa malalamiko mengi ya wananchi ikiwemo rushwa, ucheleweshaji wa haki kwani haki ikicheleweshwa ni sawasawa na haki kukataliwa," alisema Dk.Chana

Pia, alisema mifumo hiyo itasaidia kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani na majalada ya upelelezi katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka nchini.

"Mifumo hii pia itasaidia kupunguza gharama za usafirishaji wafungwa kwani kupitia TEHAMA watweza kusikilizwa wakiwa Magereza, "alisisitiza.

Alisema mifumo hiyo itasadia wananchi ambao wanahitaji kufungua mashauri yao wakiwa katika maeneo yao bila kusafiri.

"Huku nyuma mtu alikuwa akitaka kufungua kesi yake analamzimika kusafiri kutoka eneo moja kwenda jingine na kusababisha shughuli zake kusimama, lakini kwa sasa huduma zote zipo kiganjani kwake, " alisema na kuongeza kuwa: " Pia zamani mtu akitaka faili inalazimika kutumia siku mbili lakini hivi sasa anabonyeza tuu batani."

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mary Makondo alizitaja taasisi zilizopataiwa vifaa hivyo kuwa ni Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Magereza na Taasisi ya Afya ya Akili Mirembe.

Mary alisema lengo la kutoa vifaa hivyo kwa taasisi hizo ni kuongeza ufanisi katika kuharakisha utoaji haki kwa wananchi na kuondoa malalamiko yaliyopo.

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Sylvester Mwakitalu, aliishukuru serikali na kuahidi kuvitumia vifaa hivyo kuboresha utendaji kazi wa ofisi yake.

"Nikushuru wewe waziri pamoja na wizara yako kwa msaada huu utatusaidia kuboresha kazi zetu na kuhakikisha haki za wananchi zinapatikana kwa wakati na tunaahidi vifaa hivi  tutavitunza," alisema Mwakitalu



HABARI MBEYA

# TIC yazidi kuwanoa wazawa kuwekeza

**Na Nerbart Msokwa,** MBEYA

KITUO cha Uwekezaji nchini (TIC) kimeendelea na kampeni yake ya kuhamasisha wawekezaji wa ndani kuwekeza kwenye miradi na kuondoa dhana ya upendeleo kwa wawekezaji wa kigeni miongoni mwa jamii.

Meneja Uhamasishaji wa Uwekezaji TIC, Felix John akizunguza juzi wakati wa mafunzo maalumu ya uwekezaji kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya,alisema hamasa imeanza kuongezeka kwa wawekezaji wa ndani kuitikia wito wao.

Alisema wameamua kuwafikia wafanyabiashara nchini kwa lengo la kusikiliza kero zinazowakwamish kwenye uwekezaji na kuzitatua.

Vilevile, alisema lengo lingine la kukutana na wafanyabiashara hao ni kuwaelekeza dira ya uwekezaji wa ndani ambayo imeandaliwa na kituo hicho.

"Serikali haifanyi biashara ila inao wananchi wake wanaofanya biashara, hivyo tumeamua kuwafikia ili tusikilize kero na kuzitatua lakini kuwapa dira mpya, Mbeya inayo maeneo mengi ya uwekezaji hivyo tumieni hii fursa" alisema Felix.

Kaimu Meneja wa TIC Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Deusidedit Hokororo alisema mbali na kutoa elimu kwa wawekezaji hao, wanaendelea kuwasajiri na miradi wanayowekeza.

Alisema kituo hicho kina jukumu la kusimamia, kuratibu na kuwezesha wawekezaji kupata maeneo ya kuwekeza na kuhakikisha mazingira yanakuwa rafiki.

"Gharama ya kujisajili ni dola 1,100, ambapo mteja atakuwa na faida nyingi ikiwamo misamaha ya kodi, tumejipanga kuwafikia wawekezaji wetu popote na kuwapa elimu ya uwekezaji wa ndani ili wachangamkie zaidi fursa," alisema Hokororo.

Akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alisema serikali ya mkoa huo ipo tayari kutoa ushirikiano kwa wawekezaji watakaojitokeza kwenye miradi mbalimbali.

Alisema Mbeya ni miongoni mwa maeneo yenye mazingira mazuri ya uwekezaji, hali nzuri ya hewa, ardhi ya kutosha na ulinzi imara.

"Tunatamani kuona wawekezaji wetu wa ndani wakipiga hatua kama walivyo wanaotoka mataifa ya nje, sisi serikali tupo tayari kutoa ushirikiano kwa yeyote mwenye uhitaji wa kuwekeza katika sekta yoyote ikiwemo viwanda," alisema Malisa.

Baadhi ya wafanyabiashara walioshiriki mafunzo hayo waliupongeza uongozi wa TIC kwa kuendesha mafunzo hayo wakieleza kuwa yatawasaidia kuchangamkia fursa za uwekezaji kama ambavyo serikali inataka.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Aminatha Charles kutoka Chama cha Wawekezaji Wanawake Tanzania (TWC), alisema kampeni hiyo imekuja muda mwafaka na kuondoa dhana ya kuwakumbatia wawekezaji kutoka nje.

Alikishauri kituo hicho kuendelea kutoa elimu hasa ya faida ya kujiunga na kuondoa misamaha ya kodi ili kuwasaidia wafanyabiashara nchini.



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Mjumbe wa Halmashauri Kuu (NEC) ya CCM Taifa Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Silanga, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza juzi. **PICHA IKULU**

# TARURA wabanwa kuondoa kero za barabara

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Njombe mkoani hapa, ameagizwa kuondoa kero ya kukatika mawasiliano kwa baadhi ya barabara ili zipitike wakati wote.

Agizo hilo limetolewa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Filoteus Mlingo wakati akifunga mkutano wa baraza la madiwani kujadili taarifa za kata.

Mligo, aliwataka TARURA kuhakikisha wanafanya mawasiliano na uongozi wa kata ili kurahisisha utendaji wao na kuwataka makandarasi kuhakikisha wanaripoti kwenye maeneo ya kazi kwa barua kwa viongozi wa kata na madiwani.

"Watu wa TARURA barabara zetu huko ni chafu na ni mbaya, kwa mfano barabara ya Zengerendete, Utalingolo, Kisilo kwenda Luponde, mkandarasi ameanza kulima ameharibu baadhi ya eneo limekatika, sasa maeneo yale ni kwenda kuona tuone namna gani ya kurekebisha haraka," alisema Mligo.

Mligo aliitaka jamii kutunza mazingira na kufanya usafi kwenye maeneo yao ya makazi ili kudhibiti kutokea magonjwa ya mlipuko.

"Kwa kipindi hiki cha mvua ni ambacho kinaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa, hivyo jamii ichukue tahadhari kwa kuhakikisha mazingira tunayatunza na kuwa safi wakati wote," alisema Mligo.

Aliwataka madiwani kuhakikisha wanafuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuwa karibu kamati za ujenzi ili kuhakikisha inakamiila kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

Diwani wa Kata ya Luponde, Ulrick Msemwa, alisema kutokana na ufinyu wa bajeti ni vema TARURA kuhakikisha barabara zinatenezwa kwa ubora ili zidumu kwa muda mrefu.

Diwani wa Kata ya Uwemba, Jactan Mtewele, alisema ni vizuri TARURA wapate fursa ya kukaa na wenyeji ili kufahamu wakati sahihi na maeneo ambayo yanahitaji matengenezo haraka na kuondoa kero kwa wananchi..

# Wanging'ombe wanyosheana vidole kwa ukame

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

UKATAJI ovyo miti kwa ajili ya matumizi ya kuni, mkaa na shughuli za kilimo, umesababisha ukame na ukosefu wa maji kwa baadhi ya maeneo ya wilayani hapa Mkoa wa Njombe.

Erika Gyaka, mkazi wa wilaya hiyo, alisema kitendo cha kukata miti ovyo kupata maeneo kwa ajili ya kilimo ni sababu kubwa ya kutokea kwa mabadiliko ya tabia nchi na kupelekea mvua kutonyesha kwa wakati.

"Zile mvua ambazo tulikuwa tunazitegemea hazipo, mvua ni kidogo sana, yote hiyo inatokana na kukata miti," alisema Gyaka.

Valentino Mgaya, alisema licha ya kupewa elimu ya kutunza miti na mazingira, kuna baadhi wanakaidi na kuendelea kukata miti ovyo kwa shuguli za kibinadamu.

Ofisa Kilimo wa Shirika la Maendeleo ya Kilimo Mkoa wa Njombe, Ernest Ng'umbi, alisema wametoa miche 560 kwa wananchi zaidi ya 150 na kupanda kwenye maeneo ili kukabiliana na changamoto hiyo.

Mkurugenzi wa Shirika la Nado Mkoa wa Njombe, Jonathan Ngilangwa alizitaka kamati za mazingira vijijini kuhamasisha wananchi kupanda miti badala ya kutoa vibali vya kukata miti.

Mtaalamu kutoka Ofisi ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Abroni Komba, aliwataka wananchi ambao wamepokea miche hiyo kuitunza ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira..

**"Zile mvua ambazo tulikuwa tunazitegemea hazipo, mvua ni kidogo sana, yote hiyo inatokana na kukata miti," alisema Gyaka.**





# Mwinyi kusaini sheria mpya leo kuwaapisha mawaziri, manaibu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi anatarajiwa kusaini sheria mbalimbali na kuwaapisha mawaziri na manaibu waziri aliowateua hivi karibuni katika viwanja vya Ikulu leo visiwani hapa.

Dk. Mwinyi kwa mara ya kwanza atasaini hadharani sheria hizo, ikiwemo sheria mpya ya Uwekezaji Zanzibar ya mwaka 2023.

Kwa mujibu wa taarifa ya msemaji mkuu wa serikali na mkurugenzi wa mawasiliano Ikulu, Charles Hilary sheria, inakuja kupanua wigo na fursa za uwekezaji katika maeneo huru ya kiuchumi kulingana na mahitaji yaliyopo.

Alisema sheria hiyo pia itaweka miongozo ya uanzishwaji wa mifumo jumuishi ya kusimamia shughuli zote za uwekezaji ili kuimarisha ufanisi, uwazi, uwajibikaji na kuondoa urasimu katika utoaji huduma kwa wawekezaji.

Dk Mwinyi atasaini sheria namba 9 ya Mahakama ya Kadhi ya mwaka 2023 na nyingine namba 9 ya mahakama hiyo ya mwaka 2017.

Vilevile, atasaini sheria ya Mkaguzi wa Umma inayofuta sheria ya uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Zanzibar.

Hiraly, alisema baada ya hafla hiyo pia Rais Dk Mwinyi atawaapisha mawaziri na manaibu waziri aliowateuwa hivi karibu.

Miongoni mwao ni Mudrik Ramadhan Soraga aliyeteuliwa kuwa waziri wa utalii na mambo ya kale, Ali Suleiman, wa nchi ofisi ya rais Ikulu na Shabani Ali Othman, waziri wa uchumi wa buluu na uvuvi .

Wengine ni manaibu waziri, Juma Makungu Juma wa Fedha na Mipango, Salha Mohamed Mwinjuma, Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Zawadi Amour Nassor, Maji, Nishati na Madini.

Dk. Mwinyi atawaapisha viongozi hao baada ya kufanya uteuzi huo Januari 27, mwaka huu kutokana na kuridhia ombi la aliyekuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mohame Said Simai kujiuzulu hivi karibuni.



Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa CCM Ofisi ya Zanzibar, Tunu Juma Kondo, akizungumza na waandishi wa habari katika Ofisi Kuu ya chama hicho Kisiwandui Mjini Unguja jana, wakati akitoa pongezi kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kufuatia uteuzi alioufanya hivi karibuni katika Baraza la Mawaziri ulioongeza idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 4,579 waugua macho visiwani Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAGONJWA 4,579 wamepatiwa matibabu ya ugonjwa wa macho mekundu katika vituo vya afya na hospitali visiwani hapa baada ya kuripotiwa kuibuka Tanzania Bara hivi karibuni.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kasi ya maambukizi ya ugonjwa huo visiwani hapa.

Hafidh, aliwataka wananchi kuacha kutumia dawa za kienyeji kutibu ugonjwa huo na badala yake wawahi hospitali na kwenye vituo vya afya ili kupata tiba sahihi.

Naibu huyo, aliwataka wananchi wanaopata ugonjwa huo, kwa mfanyakazi wasiende ofisini na mwanafunzi shuleni hadi watakapopata tiba na kupona.

Alisema ugonjwa huo unasambaa na kupelekea maambukizi kwenye ngozi nyembamba inayozunguka gololi la jicho na kioo ambayo husababishwa na kirusi cha kiitwacho adenovirus.

"Ugonjwa huu uliripotiwa katika mikoa ya Tanzania Bara wiki mbili zilizopita na kutokana na mwingiliano ya wananchi wetu mara kwa mara, umeshaingia hapa visiwani na wagonjwa wameshaanza kuripotiwa katika mitaa mbalimbali, " alisema Naibu waziri huyo.

Alisema ni muhimu wanachi kutambua hakuna dawa yeyote ya kutibu ugonjwa huo bali matibabu yake yanalenga kupunguza makali na dalili.

"Maambukizi hutokea mara moja kwa kugusa au kushika maji maji ya mtu aliye na uambukizi wa maradhi haya kama vile matongo tongo na machozi, "alisema.

Alisema kupeana mikono na mtu mwenye maambukizi au kugusa sehemu ya kitu ambacho kimeguswa na mtu huyo kuna hatari ya kusambaa kwa mtu mwingine

kuanzia siku moja hadi tano za maabukizi.

Alizitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni jicho kuwa jekundu, kuwasha na kuchomachoma, mifuniko ya macho kuvimba, macho kuogopa mwangaza , kutoa matongotongo meupe au ya njano, kufanya ukungu kwa uoni, maumivi na mafua makali.

"Miongoni wa mambo ya kuzingatia ni usitumie dawa za asili au za kisunna, tumia maji baridi kunawia uso mara kwa mara," alisema.

Mratibu wa huduma za msingi ya matibabu ya macho, Rajab Mohammed Hilal alionya kuwa athari za muda mrefu za ugonjwa huo ni kupoteza uoni wa macho kwa sababu virusi hivyo vina uwezo wa kushambulia kioo cha jicho.

Alisema wagonjwa wengi wa macho hawafiki hospitali kupata matibabu na huishia kutumia dawa za asili.

# 'Asilimia 80 wanaminyoo Pemba'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ASILIMIA 80 ya wananchi Kisiwani Pemba na asilimia 60 Unguja wanakabiliwa na tatizo la minyoo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu maradhi yasiopewa kipaumbele, Mratibu wake kwa Zanzibar, Dk. Shaali Ame alisema jamii ya Zanzibar imeathiriwa sana minyoo.

"Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), watu walioathirika na minyoo ni milioni mbili na tatizo hili lipo zaidi kwa nchi masikini zenye kipato cha chini," alisema.

Alisema maradhi mengine yasiyopewa kipaumbele yanayoathiri jamii katika visiwa hivyo ni kichocho i kwa njia ya mkojo, matende, vikope na trakoma.

Alisema Serikali imefanikiwa kupunguza kichocho na kufikia chini ya asilimia 1.7 na matende asilimia 3.5.

Alisema wizara hiyo imekuwa ikipambana na maradhi hayo yasiyopewa kipaumbele kwa kutoa dawa na kinga katika jamii.

Pamoja na kutoa dawa na kinga kwenye jamii na shuleni, imekuwa ikipambana na konokono, kutoa elimu ya afya, kuhamasisha usafi wa mazingira, ujenzi na utumiaji wa vyoo.

Aliwataka wananchi kutumia dawa zinazotolewa kwwa jamii na kufuata kanuni za kujikinga na maradhi hayo hatimaye kuyatokomeza.

"Kuwepo kwa maradhi haya kumetofautiana baina ya Kisiwa na Kisiwa (Unguja na Pemba) au Wilaya na Wilaya, mfano hakuna maambukizi ya kichocho kwa Wilaya ya Kusini Unguja, lakini katika Wilaya hiyo kuna kiasi kikubwa cha maambukizi ya matende ikilinganishwa na wilaya nyingine za Zanzibar, " alisema.

Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, alisema kuna sababu za kuibuka kwa maradhi hayo.

Hafidh, alisema kwa mujibu wa tafiti, maradhi hayo huzipata zaidi nchi masikini kwa sababu ya ukosefu wa huduma muhimu ikiwemo maji safi na salama.

Alisema wizara hiyo itaendelea kuchukua juhudi za kupambana na maradhi hayo ili kuyatokomeza katika visiwa hivyo.

(WHO) liliamua kuitambua Januari 30 ya kila mwaka kuwa ni siku ya maradhi hayo duniani.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**TULIZO DAVID MALAVANU,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha KIDATO CHA SITA chenye index no **S0233/0579** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Secondari **ST. MARY'S MAZINDE JUU** Mwaka 2006. Yeyote atakaekiona ataoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI: **WMB/RB/8820/19**

## KUPOTEA KWA VYETI




**DISMAS STIVIN NGOTI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1597/0070/2015** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MBOKOMU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0156/0602/2018** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TANGA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/12692/2024 : PHQ/DAR/KIN/12723/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ANETH EMMANUEL NYENYEMA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba TAE 074675 iliyotolewa makao makuu ya DAR ES SALAAM mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/ILA/13863/2024**

## KUPOTEA KWA NYETI



**THOMAS LAZARO MOLLEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S0679.0154** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIMANDOLU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016, Cheti cha kuhitimu kidato cha sita chenye index No. **S2427/0647** Kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa Kupitia **ISONGOLE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018, cheti cha Chuo kilichotelewa na **SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE** Degree level mwaka 2021. Vyeti hivi vimepotea mkoa wa Arusha. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/529/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MOHAMED FUNDI MOHAMED,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha Kidato cha Nne chenye Index No S.5559-0084 Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari Singland Mwaka 2020, Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
**TAARIFA YA POLISI: PHQ/MAN/MBU/510/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALEX PAULO NASIRIRIMIKA**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba T 813 BQR. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: TAR/RB/94/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANJELA MOHAMED NGOZOMA**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari **(TOYOTA LANDCRUSER)** yenye namba za usajili **T 920CND,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**PHQ/MOR/MOR/2313/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANDREW PETER MTEI**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 833 CRD** aina ya **TOYOTA LANDCRUISER.** Chassis namba **JTFLJ73J586041005.** Engine namba **IHZ0263910.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:
**KIG/TR/RB/29/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**MOHAMED KAAYU PARSEKO,**
Anatangaza kupotea kwa Kadi ya Trekta yenye no za Usajili **T.353 CRA** Yenye CHASIS NO **BC71016113NCPLH18,** ENGINE NO **47346001000584.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/MAN/KIT/71/2024**

### THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP 117)

**DEED POLL ON CHANGE OF NAME**

**By this DEED I, BERTHA FRANCIS KAVISHE** of **P.O.Box 72466** Dar es salaam do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former name **BETRANDA FRANCIS KAVISHE** and in lieu thereof do assume and adopt this 31st day of January, 2024 the name **BERTHA FRANCIS KAVISHE,** That I change the said names due to my academic certificates which appears **BERTHA FRANCIS KAVISHE** and the name **BETRANDA FRANCIS KAVISHE** appears on my birth certificate

**AND IN PURSUANCE** of such change of name as aforesaid, **I HEREBY DECLARE** that I shall at all times hereafter, in all records, deeds and instruments in writing and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever, use and sign the said name of **BERTHA FRANCIS KAVISHE** as my name in lieu of the former name of **BETRANDA FRANCIS KAVISHE** renounced as aforesaid.

**AND I HEREBY AUTHORISE AND HEREBY** and request all persons to designate and address me in the name of **BERTHA FRANCIS KAVISHE only.**

**IN WITNESS WHEREOF** I have executed this deed this 31st ay of January, 2024.



### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### MAHAKAMA YA TANZANIA

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KIGOMA**
**Kituo cha UJIJI Mkoa wa KIGOMA**

**Shauri la Mirathi Na. 88/2022**

**Waombaji (1) LYDIA TWAHA MTULA (2) MOHAMED ADIRIKI (3) SADA ADIRIKI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: MOHAMED ADIRIKI MOHAMED**

**Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba UNAOMBWA KUFIKA MAHAKAMANI**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 06/02/2024 saa 12:00 mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama itaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 23 Mwezi 01 Mwaka 2024.

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA KIGOMA
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO UJIJI WILAYA YA KIGOMA

### IN THE DISTRICT DELEGETE COURT OF LONGIDO AT LONGIDO

**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 4873 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GEOFREY ANDEOL SHAYO**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY NEEMA KIPAUWA LAIZER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under Rule 75 of the Probate Rules)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20th day of February 2024.
No will of the said deceased is deposited at this court.
DATED at LONGIDO this 29th day of JANUARY 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT LONGIDO
**RESIDENT MAGISTRATE.**

### DEED POLL
### CHANGE OF NAME
**(Made as per registration of documents Act CAP. 117)**

BY THIS, ROSE DOUGLAS LWOGA of ILALA – DAR ES SALAAM do hereby verify that the three names ROSE DOUGLAS LWOGA, ROSE DOUGLAS MARTIN LWOGA and ROSE LWOGA MHEKWA are my true names which have used interchangeably.

- That the other ROSE DOUGLAS LWOGA has also been formally used as it appears in NATIONAL IDENTITY CARD NUMBER 19570626-11461-0001-17
- That I have formally used the name ROSE LWOGA MHEKWA in my DRIVING LICENCE NUMBER 4000287405
- That the other ROSE DOUGLAS MARTIN LWOGA has also been formally used as it appears in my BIRTH CERTIFICATE NUMBER 00843294
- That the other ROSE LWOGA MHEKWA has also been formally used as it appears in MARRIAGE CERTIFICATE NUMBER 54291
- That the other ROSE LWOGA MHEKWA has also been used as it appears in my NMB BANK CARD NUMBER 20502521430
- That the other ROSE LWOGA MHEKWA has also been formally used as it appears in my CRDB BANK CARD NUMBER 0112005203600

BY THIS DEED POLL ROSE DOUGLAS LWOGA HEREBY absolutely renounce and abandon that names of ROSE LWOGA MHEKWA that pursuance of such change of name as aforesaid I declare that I will be known at all times hereunder in all actions and proceedings in dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the name of ROSE DOUGLAS LWOGA as my name in lieu of ROSE LWOGA MHEKWA.
I FURTHER DECLARE that all transactions, certificates, deeds and commitments that I have done in the past by using my former names of ROSE LWOGA MHEKWA are valid.
AND DO HEREBY authorize and request all persons to designate, describe and address me as by my assumed name of ROSE DOUGLAS LWOGA.
In witness wherefore, I have hereunto set my hand this 04 day of JANUARY 2024.

SIGNED and delivered at Dar es salaam
By the said ROSE DOUGLAS LWOGA
Who is known to me personally this
04 day of January 2024
BEFORE ME
Name
Signature
DEPONENT



### MAHAKAMA YA TANZANIA

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MASASI**
**Kituo cha LISEKESE Mkoa wa MTWARA**
**Shauri la Madai / Ndoa Na. 02/2024**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: JANETH NYERERE**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**
**MDAI ANAMDAI MDAIWA TSH 350,000/- AMBAZO ALIKOPA KWENYE KIKUNDI CHA UWAWAMA.**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 09 Mwezi 02 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilzwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24 Mwezi 01 Mwaka 2024.

Hakimu
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO LISEKESE

### THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP. 117)
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**BY THIS DEED I, MARY DOUGLAS NCHIMBI** a citizen of Tanzania of DAR ES SALAAM, DO HEREBY wholly, absolutely and utterly renounces, relinquish and abandon the use of my former names MARY CHALE, MARY D. CHALE and MARY DENNES CHALE and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former name of MARY DOUGLAS NCHIMBI.
The reason for the names changes is Christian marriage, after marriage I adopt and use my husband's name in some documents. The name DENNES CHALE is my husband's name as it appears in my marriage Certificate while DOUGLAS NCHIMBI is my father's name. Thus, it is my wishes to use the name MARY DOUGLAS NCHIMBI as it appears in my national identity ID card with reference number 19590515-11483-00004-19.
For the purpose of evidence of such determination, I, hereby DECLARE that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and in all action, suits and proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of MARY DOUGLAS NCHIMBI as my name in lieu of and in substitution for my former names of MARY CHALE, MARY D. CHALE and MARY DENNES CHALE.
AND I HEREBY expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of MARY DOUGLAS NCHIMBI.
IN WITNESS WHEREOF I have set my hand at Dar es salaam, and I hereon substitute my old names of MARY CHALE, MARY D. CHALE and MARY DENNES CHALE by my new name of **MARY DOUGLAS NCHIMBI.**

SIGNED and DELIVERED by the said MARY DOUGLAS NCHIMBI
DEPONENT
BEFORE:
Signature:
Address: P O Box 9572 Dsm
Qualification: Advocate



KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM,E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Rais Ruto anusurika kwenye ajali akiwa ziarani Meru

**NAIROBI,** KENYA

SENETA wa Meru, Kathuri Murungi amesimulia masaibu yaliyomkuta Rais William Ruto alipokuwa katika ziara yake kwenye eneo hilo, kwamba alipata ajali ya kuogofya nusura imuuwe baada ya gari lake kugonga shimo kubwa katikati ya barabara.

Mbunge huyo alieleza jana kuwa Rais Ruto alikuwa na bahati ya kuwa hai baada ya kisa hicho, akidokeza kuwa andapo wangekuwa kwenye mteremko gari lao lingepinduka.

"Nilimwonea huruma sana rais nilipoona gari lake limegongana na mguu wake ukiwa umechanika, hebu fikiria kama ingekuwa ni kwa mteremko tungesema nini kama taifa? Hilo ndilo tatizo ninalouliza.

"Ni bahati kwamba tulikuwa tunapanda mlima, kwa hivyo iligonga shimo na kusimama hapo. Lakini kama tungekuwa tukishuka chini kwa kasi ya msafara wa rais, sasa hivi tungekuwa tunazungumza mambo mengine," alisema.

Murugi alinyooshea kidole cha lawama Mamlaka ya Kitaifa ya Barabara Kuu ya Kenya (KenHa), akishangaa ni kwa nini walishindwa kukarabati barabara hiyo. akisisitiza kuwa serikali imetumia rasilimali nyingi kuhakikisha barabara hiyo inatunzwa, lakini hawaoni fedha hizo zikitumika.

"Kwa bahati mbaya, barabara inaweza kuwa hivi licha ya kuwa na pesa nyingi, tumetenga fedha kwa KenHa. Tumetoa pesa nyingi kwa ukarabati lakini watu hao wanatumia vifaa vya chini ya kiwango," alisema na kuongeza;

"Sijui ni akina nani labda wakijipa mikataba wasitumie hizo pesa maana hatuelewi kwanini hata wenyeji hapa hawawezi kupata kandarasi hizi ndogo ndogo," alisema.

Mbunge huyo alitoa maoni kwamba kwa sababu ni Rais Ruto, timu yake ya usalama ilisuluhisha hali hiyo, lakini mwananchi wa kawaida angechukua saa nyingi kukwama katikati ya barabara. **KTN**



Rais William Ruto akihutubia mkutano uliopita. **PICHA: MTANDAO**

## Iran, Marekani zatunishiana misuli

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amesema ameamua jinsi atakavyolijibu shambulizi la droni lililowaua wanajeshi watatu wa taifa lake na wengine kujeruhiwa huko Jordan, huku Iran ikitishia kulipa kisasi endapo hatua yoyote itachukuliwa dhidi yao.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Iran, mjumbe wa taifa hilo katika Umoja wa Mataifa (UN), Amir Saeed Iran, jana alionya kwamba Tehran itajibu ipasavyo kwa shambulio lolote dhidi ya ardhi yake, maslahi, au raia nje ya nchi.

Washington iliishutumu Iran na makundi washirika wake kwa shambulio hilo, na haikutoa maelezo yoyote kuhusu jibu la Marekani.

Kamanda wa Walinzi wa Mapinduzi ya Iran alisema kuwa nchi hiyo itajibu tishio lolote kutoka kwa Marekani, akielezwa kuwa "Tunasikia vitisho kutoka kwa viongozi wa Marekani na tunawaambia kwamba tayari wametujaribu na tunafahamiana, hivyo tishio lolote halitapita bila majibu".

Ilielezwa kuwa wanajeshi kadhaa wa Walinzi wa Mapinduzi ya Iran waliuawa kutokana na shambulio la Israel huko Syria, na uvamizi wa hivi karibuni uliogonga kituo cha ushauri wa jeshi la nchi hiyo na kuua wawili, huku balozi wa Iran huko Damascus akikanusha kwamba waliokufa hawakuwa taifa hilo.

Pia ilielezwa kuwa Januari 15, mwaka huu, Iran ilishambulia kile ilichoelezea kama makao makuu ya kijasusi ya Israel katika makao makuu yake ya jimbo la kurdistan nchini Iraq. **BBC**

## Uhuru warejea kwa kiongozi wa upinzani Zimbabwe

**HARARE,** ZIMBABWE

KIONGOZI wa upinzani wa Zimbabwe, Job Sikhala, ambaye amekuwa kizuizini kwa zaidi ya miezi 18, ameachiliwa huru kutoka jela baada ya mahakama ya Harare kumpa kifungo cha nje.

Sikhala mwenye umri wa miaka 51 na ambaye ni mkosoaji mkubwa wa serikali ya Zimbabwe, ni miongoni mwa viongozi mashuhuri kukamatwa katika miaka ya karibuni, kutokana na kile mashirika ya kutetea haki za binadamu yanasema ni msako dhidi ya wapinzani kwenye taifa hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari muda mchache baada ya kuachiliwa Sikhala, alisema "Wale walionizuia kwenye jela hii kwa muda mrefu ni vyema wafahamu kwamba nipo tayari kulipia gharama yoyote ile kutokana na upendo mwingi niliyo nao kwa taifa langu".

Ilielezwa kuwa awali Sikhala pamoja na mbunge wa sasa wa upinzani Godfrey Sithole walihukumiwa kutokana na tuhuma za kuchochea umma. Na kwamba kwa sasa wamepewa kifungo cha nje cha miaka miwili kila mmoja, huku ikielezwa kuwa kundi dogo la wafuasi wao likusanyika nje ya mahakama kusherehekea uamuzi huo. **VOA**

# Asimulia kifo cha utata kilivyomkuta mwanafunzi

**NAIROBI,** KENYA

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Upili ya Wavulana ya Kilungu, Geoffrey Muema, kwa mara ya kwanza, amezungumza kuhusu kifo cha kutatanisha cha mmoja wa wanafunzi wake.

Katika video inayosambaa katika mitandao ya kijamii iliyopakiwa na Soo TV, ilionyesha kwamba mkuu wa shule alimtaja marehemu kama Emmanuel Kirimi, ambaye alikuwa amejiunga na taasisi hiyo siku 10 kabla ya kifo chake.

"Mwanafunzi huyo alilalamika kuumwa tumbo siku ya Jumatano, Januari 26, mwaka huu, majira ya saa 10:40 asubuhi, alimtaarifu kasisi wa shule hiyo ambaye alikuwa wa kwanza kukutana naye na kumshauri anywe maji kwanza kwa kuwa mipango ya kuwatayarishia kiamsha kinywa ilikuwa ikiendelea," alisema Muema.

Kwa mujibu wa Muema, mwanafunzi huyo wa kidato cha kwanza aliomba mmoja wa wanafunzi wenzake ampeleke msalani. "Waliporudi, mwanafunzi huyo alizimia na wanafunzi wenzake mara moja wakaarifu usimamizi wa shule. Mara moja naibu mkuu wa shule alinijulisha, nikamwagiza mmoja wa walimu kumkimbiza hospitali. Wakati huo kijana alikuwa amezimia," alisema Muema.

Aliongeza kuwa hospitali hiyo iko umbali wa mita 800 kutoka shuleni. Akieleza kuwa mwalimu huyo aliambatana na wengine wawili.

"Walipofika hospitalini baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kina, mtoto huyo alithibitishwa kufariki, daktari alinipigia simu na kunitaka niende hospitali haraka, nilipofika nilithibitisha kuwa kweli mwanafunzi huyo amefariki," alieleza Muema.

Alieleza kuwa baada ya kutoa taarifa kwa polisi, mara moja alirejea shuleni na kutoa taarifa kwa mwenyekiti wa wakurugenzi wa taasisi hiyo na wazazi wa marehemu.

"Mmoja wa wazazi wa marehemu alifika majira ya saa 11 jioni. Kwa msaada wa kasisi, wazazi hao waliwajulisha wanafamilia wengine wawili wa karibu waliofika kuutazama mwili wa marehemu," alisema.

Mkuu wa shule hiyo alisema familia iliomba mwili wa marehemu uhamishwe hadi katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Chiromo ili uchunguzi ufanyike mbele ya daktari wao.

"Tumerekodi taarifa na DCIO, ambaye anafanya uchunguzi kubaini chanzo cha kifo hicho. Familia imeahirisha tarehe ya upasuaji wa maiti. Lakini ikumbukwe kwamba hatuna wanafunzi shuleni ambao wana majeraha," alisema.

Aidha, ilielezwa kuwa baba wa marehemu alipoteza fahamu na kuanguka katika ofisi ya mkuu wa shule baada ya kupata taarifa hiyo ya kusikitisha. **KTN**

HABARI MICHEZO

# MAKOCHA SIMBA QUEENS, FOUNTAIN, TAMBO ZATAWALA

**Na Saada Akida**

UTAMU wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania unazidi kukolea baada ya makocha wa Simba Queens na Fountain Gate Princess kutambiana kila mmoja anaamini timu yake itavuna pointi tatu muhimu, imefahamika.

Fountain Gate Princess wanatarajia kuwakaribisha Simba Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Tayari kikosi cha wachezaji 24 wa Simba Queens kimeondoka Dar es Salaam jana asubuhi kuelekea Dodoma tayari kwa mchezo huo wa raundi ya saba.

Wageni Simba Queens watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu nzuri ya ushindi mnono wa mabao 7-0 waliopata dhidi ya Alliance Girls wakiwa nyumbani.

Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema timu yake imefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo na wanakwenda Dodoma kupambana kusaka alama tatu muhimu ili kufikia malengo yao.

Mgosi alisema licha ya kutambua ugumu wa mechi hiyo kutokana na ubora wa Fountain Gate Princess, lakini anaamini uzoefu wa nyota wake utawasaidia kucheza kwa tahadhari na hatimaye kuondoka na ushindi.

„Hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu ya ubora wa wapinzani wetu, mara ya mwisho tuliwafunga, hii ni mechi nyingine na tumejipanga katika kila idara kwa ajili ya kuvuna alama zote tatu dhidi ya Fountain Gate Princess," alisema Mgosi.

Naye Kocha Mkuu wa Fountain Gate Princess, Masoud Juma, alisema wamejipanga vyema na safari hii hawatakubali kupoteza tena dhidi ya Simba Queens.

Juma alisema amewaaandaa vijana wake kucheza kwa kujituma na vile vile kuongeza umakini kwa kutumia kila nafasi watakayotengeneza wakiwa kwenye uwanja wao wa nyumbani.

Alisema wanatambua ubora wa Simba Queens na uwezo wa wachezaji mmoja mmoja, hivyo wamefanyia kazi mapungufu yao na sasa wako tayari kukabiliana na Wekundu hao wa Msimbazi kwa kutoruhusu kufungwa wakiwa kwenye ardhi ya Dodoma.

"Safari hii tumejipanga vizuri tumefanyia kazi mapungufu yetu na ubora wa wapinzani wetu ili kutoruhusu kufungwa, tunawaheshimu Simba Queens ila hatuwagopi, tunapambana nao kuhakikisha tunafanikiwa kupata alama muhimu," alisema Masoud.



Kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), kikiwa kwenye Uwanja wa Mwalimu Julius Nyerere kuwafuata wenyeji Zambia kwa ajili ya mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia (U-17), itakayochezwa keshokutwa nchini humo. **PICHA: TFF**

# Jamhuri, Maendeleo vitani Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Jamhuri inatarajia kuikaribisha Maendeleo FC katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Gombani ulioko Kisiwani Pemba.

Ligi hiyo inarejea baada ya kusimama kwa zaidi ya mwezi mmoja kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi yaliyomalizika kwa wenyeji Mlandege kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Mechi nyingine ya leo itakuwa ni kati ya Maafande wa Zimamoto dhidi ya Wanajeshi wenzao wa Mafunzo kwenye Uwanja wa Mau B huku ushindani unatarajiwa kuonekana wakati vinara wa msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16, JKU watakapoumana na New City FC.

JKU anaongoza ligi hiyo akiwa na pointi 36 anafuatiwa na Zimamoto yenye pointi 30 na KMKM ambao ndio mabingwa watetezi wako katika nafasi ya tatu baada ya kufikisha pointi 29.

Timu nne ambazo zipo katika mstari mwekundu wa kushuka daraja hadi sasa ni Malindi FC yenye pointi 15, Jamhuri wenye pointi sawa nafasi ya 14, Ngome ipo nafasi ya 15 ikiwa na pointi 12 huku Maendeleo wenye pointi 11 wanaburuza mkia.

## Malindi yaitangazia hatari Kipanga FC

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WEKUNDU wa Mji Mkongwe, Malindi SC wanaendelea kujiimarisha ili kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Kipanga itakayochezwa Jumamosi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa Malindi, Suleiman Mohamed "Mo" alisema lengo lao ni kuhakikisha wanarudi na nguvu katika mzunguko wa pili wa ligi hiyo kwa kupata matokeo mazuri.

Mo alisema hawezi kuzungumzia matokeo ya mzunguko wa kwanza na sasa anaangalia hapa alipoanzia ili kurejesha nguvu katika kikosi chake.

Aliongeza anatarajia kushirikiana na kocha Mkuu, Abdulghani Msoma, kuhakikisha timu hiyo inamaliza kwenye nafasi nne za juu katika msimamo wa ligi hiyo.

Alisema hana wasiwasi na kikosi chake ambacho kina pointi 15 mkononi katika kupata matokeo mazuri kutokana na mwenendo uliopo baada ya kuridhishwa na viwango vya wachezaji wake kupitia michezo mbalimbali ya kirafiki waliyocheza.

## Mtibwa kurejea kivingine Ligi Kuu

**Na Oliver Albert**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema timu yake itaanza mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imara zaidi ili kujinasua mkiani katika msimamo wa ligi hiyo.

Mtibwa Sugar inaburuza mkia na pointi nane baada ya kucheza michezo 14, imeshinda miwili, imepoteza 10 na kutoa sare mara mbili.

Timu hiyo ndio iliyoongoza kuruhusu mabao mengi hadi sasa ikiwa imefungwa mabao 29 huku pia ikiongoza kwa kupoteza michezo mingi zaidi (10).

„Inaumiza kuwa mkiani katika msimamo wa ligi na ndio maana tunapambana kila mara kusahihisha makosa yetu ili tuweze kutoka hapo. Dirisha dogo tumejaribu kujiimarisha ili kushinda michezo mingi iliyo mbele yetu itakayotuwezesha kutoka katika nafasi tuliyopo sasa na kupanda juu," alisema Katwila na kuongeza.

Katika dirisha dogo Mtibwa Sugar imewaongeza kipa raia wa Burundi, Justin Ndikumana, beki Laurent Alfred, kiungo Nassor Kapama, washambuliaji Charles Ilamfiya na Rashid Juma.

## ZISIKUPITE

### PSG YAMTAKA RASHFORD

KLABU ya Paris St-Germain wanafikiria kufufua nia yao ya kumnunua mshambuliaji Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 26 kutoka Manchester United. **(The i)**

### FULHAM NA BROJA

FULHAM wanatumaini kupata hata kwa kuchelewa mshambuliaji wa Albania Armando Broja mwenye umri wa miaka 22, ingawa bado hawajakaribia dau la pauni milioni 50 la Chelsea. **(Telegraph)**

### BENRAHMA ANUKIA WEST HAM

KLABU ya West Ham imekubali kumuuza winga wa Algeria, Said Benrahma mwenye umri wa miaka 28, kwa klabu ya Ufaransa ya Lyon kwa pauni milioni 15, huku kiungo wa kati wa Hispania, Pablo Fornals mwenye miaka 27, pia akikaribia kuondoka katika klabu hiyo na kujiunga na Real Betis. **(Mail)**

### SAID KWA MKOPO

EVERTON wanaweza tu kuwasilisha ombi la mkopo kwa West Ham kwa Said Benrahma, ambaye amepewa mwanga wa kuondoka na Kocha David Moyes. **(Football Insider)**

### A'VILLA, MORGANS SAFI

ASTON Villa wamekubali mkataba wa pauni milioni 16 kumsaini winga wa Middlesbrough, Morgan Rogers mwenye miaka 21. **(Sky Sports)**

### KEAN BASI TENA

MSHAMBULIAJI wa Juventus na Italia, Moise Kean mwenye umri wa miaka 23, ameshuhudia uhamisho wa mkopo uliopendekezwa kwenda Atletico Madrid ukikwama kutokana na kuporomoka kwa kiwango chake. **(ESPN)**

### ZARAGOZA AWINDWA BAYERN

KUTOKANA na jeraha la winga wa Ufaransa Kingsley Coman mwenye miaka 27, na kuwaacha Bayern Munich wakikosa chaguo, mabingwa hao wa Ujerumani wanajaribu kusogeza mbele uhamisho wa winga wa Hispania, Bryan Zaragoza mwenye miaka 22, kutoka Granada. **(Bild)**

### PELLISTRI AKARIBIA

KLABU ya Granada wanakaribia kukamilisha mkataba wa mkopo kwa winga wa Manchester United na Uruguay, Facundo Pellistri mwenye miaka 22. **(Athletic)**

### UNITED NA MKURUGENZI MPYA

KLABU ya Manchester United inatarajia kumteua mkurugenzi mpya wa kandanda siku chache zijazo. **(Telegraph)**

### CHALOBAH HAKIELEWEKI

FULHAM, Crystal Palace na Nottingham Forest zimevunjwa moyo kumnunua beki, Trevoh Chalobah kwa bei ya pauni milioni 25 inayodaiwa na Chelsea. **(Teamtalk)**

### DIALLO AITAJA SUNDERLAND

WINGA wa Manchester United na Ivory Coast, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 19, ana nia ya kurejea Sunderland kwa mkopo hadi mwisho wa msimu huu na amewatafuta wakuu wa Old Trafford kujaribu kutilia mkazo uhamisho huo. **(Football Insider)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# INAUMA KUONA WACHEZAJI SENEGAL WAKILIA - CISSE

Kocha huyo amesema ilikuwa ngumu kwenye vyumba vya kubadilishia nguo baada ya...

**ABIDJAN, Ivory Coast**

KOCHA wa Senegal, Aliou Cisse, amesema „ilikuwa ngumu kutazama wachezaji wakilia" kwenye vyumba vya kubadilishia nguo baada ya kushindwa kwa mikwaju ya penalti na Ivory Cost katika hatua ya 16 bora ya Kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON.

Mabingwa hao watetezi walitupwa nje kwa mikwaju ya penalti 5-4 na wenyeji wa michuano hiyo Jumatatu kufuatia sare ya 1-1 baada ya muda wa ziada.

„Nimesikitishwa baada ya matokeo haya, haswa kwa wachezaji wetu. Tulikuja hapa kutetea taji na kuwapa furaha watu wetu," alisema Cisse.

Kocha huyo alisema kushindwa kwa mtindo huo baada ya kutawala mechi kulifanya maumivu yawe makali zaidi.

„Ni vigumu kuona wachezaji wakilia kwenye vyumba vya kubadilishia nguo. Mechi ilikuwa ya ajabu na ngumu, tungeweza kushinda," Cisse alibainisha.

Senegal waliongoza hadi dakika ya 86 pale Franck Kessie aliposawazisha kwa mkwaju wa penalti. Na Cisse alihisi timu yake ilishindwa kusimamia vyema mchezo wakati ilikuwa muhimu zaidi kufanya hivyo.

„Tulipoteza kwa mikwaju ya penalti, tuliendelea kuongoza hadi dakika 5 za mwisho. Nimesikitishwa baada ya kushindwa huku, hasa baada ya uchezaji wetu na mechi ya kwanza," alilalamika.


Huku jitihada zao za kutaka kutetea ubingwa wao kukwama, Cisse alikiri mabadiliko hayawezi kuepukika kwani timu inatazamia kujijenga upya.

„Tunahitaji kufanya mabadiliko baada ya kushindwa huku, tutaona kitakachotokea siku zijazo. Kuna huzuni na wachezaji wetu wana huzuni, kama ilivyo kwa watu wa Senegal," kocha huyo alikiri.

Hata hivyo, Cisse alijivunia kampeni ya Senegal ambayo haijashindwa katika hatua ya makundi. "Tulijiandaa vyema na tusisahau tuna ushindi mara 3 katika mechi 3," aliongeza.

Baada ya kushindwa kutetea taji lao kwa mtindo wa hali ya juu, Cisse anajua kwamba Senegal lazima ijitoe na kufanya kazi ili kurejea kwa nguvu zaidi.

# PEP KUAMUA KUHUSU MUSTAKABALI WAKE



**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesema atazingatia "mambo mengi" kabla ya kuamua kuongeza mkataba wake na klabu yake ya Manchester City.

Kocha huyo ana mkataba Etihad hadi mwaka 2025 na anatazamiwa kuamua kuhusu mustakabali wake baadaye mwaka huu.

Guardiola, ambaye aliona mpinzani wake wa karibu Jurgen Klopp akitangaza kuondoka Liverpool wiki iliyopita akitaja ukosefu wa nguvu ya kufanya kazi hiyo, alisema yeye "anajisikia vizuri" lakini anakiri mambo yanaweza kubadilika katika miezi michache ijayo.

"Kwa kawaida uamuzi ni wa haraka," Guardiola aliuambia mkutano wa wanahabari jana.

"Hatuwezi kukubali miaka nane ni muda mwingi, mwakani itakuwa misimu tisa, kwa hiyo ni muda mwingi. Ni lazima tuwaone wachezaji, tabia zao zikoje, viwango vyetu, kama tunaweza kuvitunza, na kama wachezaji wanakufuata, ikiwa nimechoka au lah.

"Mambo mengi yanahusika katika hilo. Kuongeza baada ya miaka miwili sio sawa na kuongeza baada ya tisa. Ni tofauti kabisa. Bado nimekaa hapa na niko sawa.

"Nadhani tuna muda sasa najisikia vizuri kama nilivyokuwa siku zote lakini soka linabadilika sana. Nina maoni yangu kwamba unapobakiza mwaka mmoja na nusu kwenye mkataba wako ni mwingi, muda mwingi kwenye soka la dunia. "

City, inayotafuta rekodi ya kutwaa taji la nne la Ligi Kuu ya England mfululizo, imekuwa na kiwango kizuri msimu huu, lakini itamenyana na Burnley Jumatano ikiwa ni nyuma ya ushindi wa mechi saba.

Mfululizo huo umejumuisha washindi wa dakika za lala salama dhidi ya Newcastle United na Tottenham Hotspur katika michezo yao miwili iliyopita na wamesalia kwenye nafasi ya kurudia mataji matatu ya msimu uliopita ya Ligi, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA.

"Kushinda kunakusaidia kuwa na nguvu zaidi, unapopoteza michezo unakuwa mchovu zaidi," alisema Guardiola.

"Ninaona timu ikiwa bora na kucheza na wapinzani wagumu kama vile Goodison Park baada ya Klabu bingwa ya dunia au Newcastle au Spurs ugenini na kuona jinsi timu ilivyokuwa, bado tuko pamoja, tuko kwenye njia moja. Hiyo inakupa nishati. Nishati huiwashi wala kuizima.

"Lazima ulete nguvu kila siku na kile unachoishi katika maisha yako ya kibinafsi na mambo mengi. Hiyo ndiyo ninayoishi sasa. Ndiyo maana nilisema mwaka mmoja na nusu ni muda mwingi."

# Arteta asifia kiwango cha Jesus

**LONDON, England**

MIKEL Arteta alisifu uchezaji wa Gabriel Jesus wakati Mbrazil huyo alifunga na kusaidia katika ushindi wa mabao 2-1 wa washikabunduki hao dhidi ya Nottingham Forest, juzi.

Jesus mwenye umri wa miaka 28, alifunga bao lake la nne pekee katika kampeni ya Ligi Kuu ya England msimu huu.

Kisha pasi yake sahihi ikamlisha Bukayo Saka kwa bao lake la pili katika mechi tatu, kumaanisha kuwa bao la dakika za lala salama la Taiwo Awoniyi kwa wenyeji lilidhihirisha faraja tu.

Arteta alifurahishwa na juhudi zake za mchezaji wake huyo pale kwenye uwanja wa City Ground.

Alisema: "Tunamhitaji sana Jesus katika ubora wake. Nilikuwa na hisia kubwa kabla ya mchezo na nikamwambia.

"Alikuwa na maji mengi kwenye goti na alikuwa akijitahidi. Alikuwa akipiga teke kila mwanafizio siku mbili zilizopita akisema, 'Nataka kuwa kwenye uwanja huo'.

"Alisukuma kila mtu kuwa pale na wakati mtu ana mtazamo huo, hamu hiyo katika wakati huu, kitu kizuri kitatokea kwa sababu ya uwezo na ubora wa kufanya hivyo. "Alikuwa mzuri leo, nimeridhishwa sana na upambanaji wake na ubora wake, nadhani."



# Sinayoko: Kuna kazi kubwa mbele yetu

**ABIDJAN, Ivory Coast**

BAADA ya kufanya kazi kubwa katika ushindi wa 2-1 wa Mali dhidi ya Burkina Faso katika mchuano wa Kombe la Mataifa ya Afrika, (AFCON), hatua ya 16 bora, Lassine Sinayoko amesema bado kuna kazi nyingi ya kufanya, lakini alifurahishwa na matokeo.

Mshambuliaji huyo anayecheza soka lake nchini Ufaransa alipongeza uimara wa timu yake dhidi ya majirani zao, lakini akaonya kwamba bado kuna kazi kubwa ya kufanywa kwani mechi zinazofuata zitakuwa ngumu zaidi.

"Ilikuwa mechi ngumu sana dhidi ya timu nzuri. Ilitubidi kufanya kazi kwa bidii zaidi, lakini ninafurahi hatimaye tulipata matokeo.

"Bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili tusherehekee ushindi huu, lakini bado tukumbuke kuwa kuna kazi kubwa mbeleni," alisema Sinayoko.

Mali watamenyana na wenyeji, Ivory Coast katika robo fainali mjini Bouake siku ya Jumamosi katika kile kinachoahidi kuwa mechi nyingine ya mtoano.



HABARI MICHEZO

# TANZANIA KICHEKO INONGA, DIARRA ROBO FAINALI AFCON

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Nchini (TPLB), imewapongeza wachezaji, Henock Inonga na Djigui Diarra, kwa kuzisaidia timu zao za taifa (DRC na Mali), kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) inayoendelea nchini Ivory Coast, lakini pia kuitangaza Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wachezaji hao wamekuwa na mchango katika kuzifikisha timu zao hatua ya robo fainali.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa bodi hiyo, Almasi Kasongo, alisema jana uwepo wa Inonga na Diarra katika michuano hiyo mpaka sasa kunaendelea kuitangaza Ligi ya Tanzania na kuonyesha imekuwa bora sana barani Afrika.

„Kwanza ni kitu kikubwa ligi yetu imetoa wachezaji ambao wamefanikisha timu zao za taifa kutinga robo fainali za AFCON.

Kwetu sisi ni kitu kikubwa na tunawapongeza sana, inaonyesha ubora wa ligi yetu na imeonyesha pia tumepiga hatua na kile tulichokuwa tunakihitaji sisi, baadhi ya waandishi wa habari na wadau wa soka, klabu zisajili wachezaji wa kigeni angalau wanaocheza timu za taifa na wenye uwezo mkubwa sasa kimeonyesha mafanikio," alisema Kasongo.

Alisema mijadala iliyokuwa inaendeshwa juu ya kusajili wachezaji wa kigeni wenye uwezo haikuwa kwa ajili ya kuziponda klabu, ila kuzisaidia zenyewe na mpira wa Tanzania ambapo leo matunda yake yameonekana.

„Ile mijadala iliyokuwa inaanzishwa katika vyombo mbalimbali vya habari na kuchangiwa kwa muda mrefu, sisi kuweka kanuni matunda yake yanaanza kuonekana, klabu zimeanza kutuletea wachezaji ambao wanaendana na ubora wa ligi yetu, waozisaidia klabu zao na kuzibeba timu zao za taifa, ni jambo kubwa kwa Bodi, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) na mpira wa Tanzania," Kasongo alisema.

Ofisa huyo alisema siku zote yeye si muumini wa kupunguza wachezaji wa kigeni kwenye ligi ili wachezaji wa Kitanzania wapate nafasi, ila anaamini kuwepo kwa wachezaji wao kunawapa fursa kujifunza na kuwa bora zaidi.

„Mimi siku zote mtazamo wangu vijana wa Kitanzania wakipata nafasi, msingi mkubwa ni kujituma, nidhamu, kupambana na kusikiliza yale ambayo walimu wanawaambia, binafsi sijawahi kuwa muumini kuonyesha ukiwa na wachezaji wengi wa kigeni katika ligi yako tafsiri yake eti wachezaji wako wa ndani wanakosa nafasi ya ushindani," alisema.

Inonga, beki wa kati wa Simba, timu yake ya DR Congo imetinga hatua hiyo kwa kuitoa Misri kwa mikwaju ya pelnati 8-7, huku kipa wa Yanga, Diarra aliwezesha timu yake ya Mali kutinga hatua hiyo kwa kuifunga Burkina Faso mabao 2-1, iliyokuwa na mchezaji mwingine anayecheza Ligi ya Tanzania, Stephane Aziz Ki wa Yanga.

## Prisons yaipigia hesabu Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons imeanza kupima afya wachezaji wake kabla ya kuingia kambini kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga itakayochezwa Februari 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Sokoine, Mbeya.

Ofisa Habari wa Prisons, Issaka Chacha, alisema kikosi hicho tayari kimeshaanza mazoezi ya utimamu wa mwili, lakini kabla hawajaanza kufanya hivyo wachezaji wote walipimwa afya ili kuangaliwa kama wanaweza kuhimili aina hiyo ya mazoezi magumu, lakini kuanza maandalizi ya mechi za lala salama.

„Unajua ligi imesimama kwa muda sasa kupisha Kombe la Mapinduzi na AFCON, sasa waliporudi wachezaji wetu wote waliingia kwenye vipimo, na sisi hatutanii tunapima kweli, sisi ni maafande," alisema Ofisa Habari huyo mpya ambaye amechukua nafasi ya Jackson Mafulango.

Alizitaja sababu za kuwapima afya wachezaji ambao tayari wamesajiliwa tofauti na klabu zingine ambazo huwapima wakati wa usajili.

„Tumepima afya za wachezaji, kwa sababu walikuwa mapumziko, kwanza tulitaka kujiridhishe je, wanaweza kuanza mazoezi ya nguvu? Kwa sababu ligi ilisimama na walikuwa mapumziko, haiwezekani kuwafanyisha mazoezi makali bila kuwapima. Nia ni kujiweka tayari na michezo yetu ya Ligi Kuu tukianza na Yanga," alisema.

Aliongeza licha ya kuondokewa na Edwin Balua aliyejiunga na Simba, wamefanya usajili wa wachezaji watano ambao wanaamini watakiongezea nguvu kikosi chao.



Wachezaji wa Azam FC wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba itakayochezwa Februari 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Gamondi: Hausung FC wametupa mwanga

INATOKA UK. 24

kitu kitaenda sawa.

"Mbali na yote naweza kusema nimepokelewa vizuri nina furaha sana kuwa sehemu ya kikosi cha Yanga, niko tayari kwa upande wangu... unajua unapokuwa ndani ya klabu kubwa lazima uwaze makubwa, nipo tayari kuisaidia timu kufanya vizuri," alisema Guede.

## Benchikha aweka msimamo wake kwa Inonga

INATOKA UK. 24

ma tatu kwenye kila mchezo.

„Ni mechi ambazo ni muhimu sana kwetu, nakiandaa kikosi changu kucheza kwa kutumia kila nafasi wanayoipata," alisema Benchikha.

Mbali na kauli hiyo ya Benchikha, Meneja Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally alisema mechi za mwezi huu ndizo zitakazoamua mustakabali wa msimu mzima wa klabu hiyo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu Tanzania.

„Ni mechi ambazo zitaamua kama tunasonga mbele kwenye hatua ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika au la, pia tutajua kama tupo kwenye mbio za ubingwa au tutakuwa tumetoka," alisema Ahmed.

Ratiba ya mwezi Februari inaonyesha Simba itaanza kibarua chake Jumamosi itakapocheza dhidi ya Mashujaa FC kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, kabla ya kwenda Tabora kucheza dhidi ya Tabora United, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Februari 6, baada ya hapo itakutana na Azam Fc Februari 9.

Baada ya mchezo huo wa Azam, Februari 12 itacheza ugenini dhidi ya Geita Gold, na siku tatu baadaye itacheza nyumbani dhidi ya JKT Tanzania, kabla ya kucheza na Mtibwa Sugar Februari 18.

Hata hivyo, mechi dhidi ya Mtibwa iko kwenye hatihati kwani inabidi isafiri kwenda nchini Ivory Coast kucheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas, Februari 23.

Michezo
Alhamisi Februari 1, 2024
Nipashe

Inauma kuona wachezaji wakilia - Cisse UKURASA 21





Kiungo wa Timu ya Taifa ya Afrika Kusini 'Bafana Bafana', Teboho Mokoena (kushoto), akiwania mpira na mchezaji wa Morocco, Ghanem Saiss, wakati wa mchezo wao wa Hatua ya 16 Bora ya Fainali za Mataifa ya Afrika juzi usiku nchini Ivory Coast, Bafana Bafana ilishinda mabao 2-0 na kutinga hatua ya robo fainali. **PICHA: MTANDAO**

# BENCHIKHA AWEKA MSIMAMO WAKE KWA INONGA

●●●Ataja Ligi ya Mabingwa Afrika, atangaza vita mechi sita Februari hii...

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Abdelhak Benchikha, ameuambia uongozi wa klabu hiyo kuwa beki wake wa kati, Henock Inonga yupo kwenye mipango yake msimu huu katika mashindano ya Kimataifa na Ligi Kuu.

Inonga ambaye kwa sasa yupo na kikosi cha timu yake ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwenye fainali za AFCON zinazoendelea nchini Ivory Coast, anatajwa kutakiwa na vilabu vya soka vya FAR Rabat na Berkane za Morocco.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Iman Kajula, alisema licha ya maneno kuzagaa kuwa nyota huyo anatakiwa nchini Moroccco uongozi bado haujapata ofa yoyote kutoka kwa timu hizo.

Hata hivyo amesema kocha wao, Benchikha ameonyesha wazi kuwa na mipango na beki huyo wa kati katika kipindi hiki ambacho klabu ipo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi na mbio za ubingwa wa Ligi Kuu na komba la FA.

„Labda niseme tu kocha wetu ana mipango yake, na katika mipango hiyo ameonyesha Inonga yupo kwenye mikakati yake, na sisi tulisema yeye kocha ndiye atakuwa na maamuzi juu ya wachezaji," alisema Kajula.

Aidha, alisema kama uongozi wanaweza wakaongea kitu pale ofa ya timu hizo zinazotajwa zitawafikia mezani kwao rasmi.

„Simba haina utaratibu wa kuzuia wachezaji kwenda timu nyingine pale ofa nzuri kwa mchezaji na kwetu inapofika, kwa sasa kocha ndiye atakayetupa ushauri, hatuwezi kuzungumzia kitu ambacho hakijaja rasmi, tusubiri tuone," alisema Kajula.

Inonga amekuwa kwenye kiwango cha juu katika michuano ya AFCON ambapo mpaka sasa amecheza katika mechi zote za timu yake na kuisaidia kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Kongo sasa inajiandaa kuumana na Guinea kwenye hatua hiyo ya robo fainali kuwania kutinga nusu fainali.

Wakati huo huo, ratiba inaonyesha Simba ina mechi saba mwezi Februari, sita zikiwa za Ligi Kuu na moja Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, akisema amewaandaa vijana wake kwa vita hiyo.

Benchikha, amesema kuwa mechi hizo ni kama vita kwake kwa mwezi huu wa Februari akipania kuvuna ala-

INAENDELEA UK. 23

## Gamondi: Hausung FC wametupa mwanga

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema mechi yao ya kombe la FA dhidi ya Hausung FC ilikuwa kipimo sahihi kwao katika harakati ya kurejesha timu kwenye michuano ya Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Juzi, Yanga ikiwa kwenye uwanja wa Azam Complex iliibuka na ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya timu hiyo na kusonga mbele katika michuano hiyo.

Gamondi alisema, baada ya kumalizika kwa Kombe la Mapinduzi huo umekuwa mchezo mzuri na kipimo katika harakati zao za kuiimarisha timu kabla ya hekaheka za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Hii ni mechi ya kutafuta matokeo lakini imekuwa kipimo kizuri kwetu kujiandaa na michezo yetu ijayo ya ligi kuu, hadi kesho (jana) baadhi ya nyota ambao timu zao zimeondolewa katika fainali za AFCON wataunga na kikosi tayari kwa ajili ya michezo ijayo, lakini huu ulikuwa mchezo muhimu," alisema Gamondi na kuongeza,

„Siangalii idadi ya magoli tuliyoyapata, nilikua naangalia mnyumbuliko wa wachezaji kuanzia wale ambao hawakuwa wakipata namba na wachezaji wengine, hii imenipa picha nini cha kufanya kwenye michezo ijayo," alisema Gamondi.

Aidha, alisema hana tatizo na namna ratiba ilivyo ambapo watakuwa wakipumzika kwa siku mbili tu kabla ya kucheza mchezo mwingine.

Kikosi cha Yanga leo kinatarajia kuelekea Bukoba mkoani Kagera kwa ajili ya mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar uliopangwa kuchezwa kesho wenye uwanja wa Kaitaba.

Wakati huo huo, mshambuliaji mpya wa timu hiyo, Joseph Guede amesema kwake kazi aliyonayo ni kuhakikisha anafanya mambo makubwa kwa kuwa yupo kwenye moja ya timu kubwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Guede alisema amefurahi kuwa sehemu ya kikosi cha Yanga ameona viongozi ni wazuri na wana ushirikiano ambao una mpa picha kuona kila

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >